# *MUHURI WA PASAKA*

Hakika ni majaliwa kuwapo hapa asubuhi ya leo, kwenye siku hii ya kuzaliwa kwa tawi hili la Wafanyabiashara wa Full Gospel hapa Phoenix, na kujua ya kwamba Bwana alinipa sehemu yake ndogo, kuwa sehemu ya ushirika huu. Ninataka kumsalimu Ndugu Carl Williams na mkewe, Ndugu Stromei, wengine hapa jukwaani, Ndugu Shores, Ndugu Outlaw, wahudumu, na ninyi nyote watu wazuri.

2 Mnajua, ni—nilikuwa na sherehe ya siku ya kuzaliwa juma lililopita, pia. Nami nina umri mkubwa kidogo zaidi tu kuliko tawi. Ninaamini yeye alisema, "Umri wa miaka mitano na . . . wa tawi hili."

3 Mtu fulani alisema, hivi majuzi, alisema, "Una umri wa miaka mingapi, Ndugu Branham?"

4 Nikasema, "Ishirini na sita." Kisha nikasema, "Nilifutilia mbali miaka ishirini na mitano ya kwanza. Sikumtumikia vizuri sana katika hiyo." Nikasema, "Ninatumaini atafuta, pia." Kumfanya Yeye afanye hivyo litakuwa ni jambo tofauti.

5 Lakini ni vizuri kuwapo hapa. Na sasa hatutaki kuchukua muda wenu mwingi. Kwa sababu sisi . . . Mimi—mimi daima huogopa, baada ya kusikia baadhi ya shuhuda hizi nzuri, na mambo yanayoendelea, ambayo mimi . . . na nyimbo, kwamba nitafanya jambo fulani litakalovuruga hayo. Nami nilitaka kuongezea kwa hayo, kama kungekuwako na jambo lolote ningeliweza kuongezea kwa hayo. Dada hawa . . .

6 Yule ndugu aliyeimba ule wimbo asubuhi ya leo, yule ndugu mweusi, niliufurahia huo, *Jicho Kwa Shorewanda*.

7 Na dada hawa walioimba wimbo huu, ambao umekuwa mmoja wa misaada yangu tangu nilipokuwa hapa mara ya kwanza. Ninao huo. Ninao kwenye santuri, na nimeucheza sana hata ukaharibika, *Ningependa Kulizungumza Kwa Undani Naye*. Nami nilimwuliza Ndugu Dawson Riley pale, rafiki yangu, kama angeweza, baadhi yao, kama wangeona kama wangewapata hao akina mama, kama bado wangalipo hapa duniani, wauimbe tena asubuhi ya leo. Nami ninatumaini Terry aliupata. Nami ninadhani aliupata. Ninataka kuutoa huo hapo, labda, kuurekodi ama chochote kile, kwa maana kweli ninaupenda huo wimbo. Na hiyo ndiyo shauku ya—yangu, ni kulizungumza hilo kwa undani naye. Nafikiri sote tunataka kufanya hivyo. Hiyo ndiyo sababu tupo hapa asubuhi ya leo.

8 Sasa, mikutano ijayo, juma lijalo. Je! ni sawa kulisema? [Ndugu mmoja anasema, "Hakika."—Mh.] Mimi—mimi nitakuwa nyumbani juma hili lijalo, kwenye maskani, Jumapili ijayo, kwa

ajili ya ibada ya Pasaka; Jumamosi usiku, Jumapili, na Jumapili usiku. Na kisha ninarudi huko California. Ninyi watu wote mlio karibu na California, hakika tutafurahi kuwa pamoja nanyi kwenye mkutano kule. Nami nafikiri Billy ametuma matangazo yasiyo sahihi. Ni . . . Yeye alisema, "Kwenye Hoteli ya Biltmore," ninaamini, "ndiko utakakokuwa." Ni . . . [Mtu fulani anasema, "Tusingeweza kupapata."] Msingeweza kupapata. Na uko huko Eastmont? ["Embassy."] Embassy, Hoteli ya Embassy. Kwa hiyo yeyote wa watu wa Full Gospel kule atawajulisha, kama mkiwa huko.

9 Na halafu tutarudi kutoka kule, na niende Afrika Kusini baada ya hapo. Mwezi mmoja tu kutoka leo, tutaabiri kwenda Afrika Kusini, tukitarajia wakati mkuu katika Bwana, kama mataifa matatu kule. Kwa hiyo hakika tu—tunaomba maombi yenu. Labda sitaweza kuwaona tena, kama Bwana atatusafirisha kwenda, mpaka nitakaporudi. Nami ninatumaini nitakuwa na ripoti nzuri sana kwa ajili yenu nitakaporudi.

10 Mara ya mwisho kule chini, nafikiri kwamba Bwana alinipa mkutano mkubwa kuliko yote niliyopata kuwa nayo. Na wakati mmoja, kwa wito wa madhabahuni . . . Sasa, huu ni kutoka kwa wenyeji wavaa mablanketi. Kadiri nijuavyo mimi, kulikuwa na elfu thelathini waliomkubali Kristo kwa wakati mmoja. Nasi tulifikiri labda walimaanisha uponyaji wa mwili, kwa sababu kulikuwa na kama elfu ishirini na tano walioponywa kwa wakati mmoja. Na kesho yake, meya wa—wa Durban, ambaye ni Sydney Smith, alisema, "Nenda kwenye dirisha lako, uangalie wakiteremka barabarani." Na kulikuwa na lori baada ya lori, yaliyojaa shehena ya magongo makuukuu ya kutembelea na kadhalika, yamelundikwa tele mpaka juu; yaliyokuwa yakiwafuata, wananchi, ambao walikuwa na vita vya wenyewe kwa wenyewe, wakishuka kwenye barabara za jiji hilo, wakiimba *Amini Tu* katika lugha yao ya kienyeji.

11 Ninawaambia, moyo wangu ulisisimkwa. Kama . . . Unapoona kitu kama hicho, Ndugu Shores, unaona kazi yako si ya bure basi. Unaona, ulijaribu. Nami ninatumaini ya kwamba Mungu atarudia jambo hilo tena, si kwa sababu—kwa sababu tunashuka kwenda kule, bali ni kwa sababu tunakutarajia kuja kwa Bwana.

12 Na kama vile wimbo ulivyosema, tunamtafuta maskini, yule kondoo aliyepotea. Huyo ndiye . . . Yeye—Yeye hatakuja mpaka kondoo huyo ameingia. Kila mmoja hana budi kuwa zizini. Hatafunga mlango mpaka huyo wa mwisho ameingia. Kwa hiyo, ndugu wahudumu, hakika niko pamoja nanyi, asubuhi ya leo, katika kujaribu kumtafuta kondoo huyo wa mwisho. Huenda akawa yuko Phoenix, asubuhi ya leo. Mimi sijui. Bali wakati huyo wa mwisho atakapoingia, ndipo Mchungaji atakapofunga mlango.

13 [Ndugu fulani anasema, “Ndugu Branham?”—Mh.] Naam? [“Naweza kusema neno moja?”] Hakika unaweza. [“Nilisahau jambo fulani. Tumekuwa tukizungumza juu ya…” Sehemu tupu kwenye kanda.] Hilo ni sawa kabisa. [“Nami ninajua, kila mtu husahau jambo fulani, wakati mwingine.”] Mimi sisahau. [“Loo!”]

14 Mimi ndimi ambaye karibu inanibidi, niandike kile nitakachosema. Mimi ni…Kwa kuwa ninazidi kuzeeka, ninapata shida kukumbuka, ninaandika Maandiko yangu, na kadhalika. Zamani ilikuwa kwamba, ningeweza kuweka kama Maandiko hamsini mawazoni mwangu, na kamwe hata nisininii…nikayapitia moja kwa moja, lakini nilipitia maili nyingi ngumu siku za nyuma.

15 Kwa hiyo, tunakutazamia kule Kuja kwa Bwana. Bwana awabariki ninyi nyote!

16 Na halafu unapanda hapa, nawe unafikiri. Unaketi hapa na kuwasikia watu hawa wakishuhudia. Unafikiri, “Vema, nitakaposimama, nitasema jambo fulani kuhusu hayo.” Ndipo, kuna mengi sana ya kusema, ungekuwa siku nzima unayasema. Lakini, kwa hakika ninawapenda ninyi nyote. Naomba tawi hili dogo liendelee kukua. Naomba kila kanisa Phoenix liendelee kukua mpaka Yesu atakapokuja, ndilo ombi langu la moyoni.

17 Sasa, nafikiri, ili tupate tu kupumzika kidogo tu, hebu na tusimame tunapoomba. Sawa?

18 Mwenyezi Mungu, Baba wa Bwana wetu Yesu Kristo, ambaye ulimfufua katika wafu, na umemtoa kwetu kama dhabihu, na Bwana na Mwokozi. Tunakushukuru sana kwa majaliwa haya tuliyo nayo asubuhi ya leo, kusimama katika Uwepo Wako, pamoja na watu Wako ambao wamekombolewa na wanatazamia Kuja Kwake mara ya pili kutukufu, kutupokea Kwake. Kama kuna dhambi miongoni mwetu, Bwana, tusafishe na hisopo Yako. Nasi tunaomba, Baba wa Mbinguni, ya kwamba utamponya kila mgonjwa aliye miongoni mwetu.

19 Na kama kungekuwako, labda, wale wasiokujua Wewe, katika ubatizo huu mkuu wa Roho Mtakatifu ambao tunaushindania sana, na kusema ni wa lazima, kulingana na Maandiko ya siku hii ya mwisho. Tunaomba, Mungu, ya kwamba atatushukia sisi sote, leo, na kutubatiza upya tuingie katika ule Mwili, na kuwaleta wale walio nje, waingie, pia, Baba.

20 Tubariki tunaposoma Neno Lako na kujitahidi kuzungumza yale yaliyo Kweli ya Neno Lako. Vifumbe vinywa vyetu kwa yale ambayo si kweli, na uifungue mioyo na vinywa vyetu kwa yale yaliyo Kweli, tunapojikabidhi Kwako. Tumia vinywa vyetu kuzungumza, na masikio yetu kusikia, na mioyo yetu kupokea. Kwa kuwa tunaomba hayo katika Jina la Yesu, Ambaye ameamuru hayo yawe hivyo. Amina.

21 Ningependa kusoma kutoka kwenye Neno Takatifu, sehemu tatu katika Biblia. Na kama ungewekea haya alama, na unataka kuendelea uyamalizie, kuyasoma kwa ajili ya maelezo zaidi, ningefurahi sana kama ungaliyaandika. Sehemu nitakazosoma ni Mathayo 28:1-10, na halafu Ufunuo 1:17-18, Warumi 8:11. Na hebu nizirudie tena. Na sasa Mathayo 28:1 hadi 10, Ufunuo 1:17 hadi 18, na Warumi 8:11.

22 Sasa tunakaribia Pasaka. Na wakati mnapofungua sehemu zenu, na kuziandika. Ninafikiri ya kwamba juma hili lijalo ndilo juma kuu sana na la kihistoria la majuma yote ya mwaka. Nafikiri ya kwamba jambo kubwa sana tutakalosherehekea juma hili, juma hili lijalo, lilikuwa ndilo tukio kubwa kuliko matukio yote yaliyopata kutukia duniani. Sidhani jambo lolote lingeweza kulizidi. Unasema, "Vema, ku—kusulibiwa kulikuwa ni kukuu." Lakini watu wengi wamekufa, watu wengi wamesulibishwa, hata katika siku zile zile za Bwana wetu. Lakini kulikuwako tu na Mmoja wao ambaye alifufuka katika wafu. Hilo lilitia muhuri jambo hilo.

23 Sasa ninataka kusoma. Na huu kwa namna fulani ni ujumbe mdogo unaotangulia Pasaka, Bwana akipenda, kama dakika arobaini hivi. Sasa hebu na tusome kutoka katika Injili ya Mathayo Mtakatifu, mlango wa 28, mwanzoni.

> *Hata Sabato ilipokwisha, ikipambazuka siku ya kwanza ya juma, Mariamu Magdalene, na Mariamu yule wa pili, walikwenda kulitazama kaburi.*
>
> *Na tazama, palikuwa na tetemeko kubwa la nchi, kwa sababu malaika wa Bwana alishuka kutoka mbinguni, akaja, akalivingirisha lile jiwe akalikalia.*
>
> *Na sura yake ilikuwa kama umeme, na mavazi yake meupe kama theluji.*
>
> *Na kwa kumwogopa, wale* wenye kutetemeka... *walinzi* (samahani) *wakatetemeka, wakawa kama wafu.*
>
> *Malaika akajibu, akawaambia wale wanawake, Msiogope: ninyi, kwa maana najua ya kuwa mnamtafuta Yesu aliyesulibiwa.*
>
> *Hayupo hapa; kwani amefufuka kama alivyosema. Njoni, mpatazame mahali Bwana alipolazwa.*
>
> *Nanyi nendeni upesi, mkawaambie wanafunzi wake, Amefufuka katika wafu. Tazama, awatangulia kwenda Galilaya; ndiko mtakakomwona. Haya, nimekwisha waambia.*
>
> *Wakaondoka upesi kutoka kaburini, kwa hofu na furaha nyingi, wakaenda mbio* na *kuwapasha wanafunzi wake habari.*
>
> *Na walipokuwa wakienda kuwapasha wanafunzi wake habari, tazama, Yesu akakutana nao, akisema,*

*Salamu! Wakakaribia wakamshika miguu,* na kumsujudia.

*Kisha Yesu akawaambia, Msiogope; enendeni, mkawaambie ndugu zangu waende Galilaya, ndiko watakakoniona.*

24 Na Ufunuo, mlango wa 1, na kifungu cha 17 na 18.

*Nami nilipomwona, nalianguka miguuni pake kama mtu aliyekufa. Akaweka mkono wake wa kuume juu yangu, akisema, Usiogope, Mimi ni wa kwanza na wa mwisho,*

*Mimi ni Yeye aliye hai; nami nalikuwa nimekufa, na tazama, ni hai hata milele na milele, Amina; nami ninazo funguo za mauti, na za kuzimu.*

25 Na katika Kitabu cha Warumi, mlango wa 8, na kuanzia kifungu cha 11.

*Lakini, ikiwa Roho wake yeye aliyemfufua Yesu katika wafu anakaa ndani yenu, yeye aliyemfufua Kristo Yesu katika wafu ataihuisha na miili yenu iliyo katika hali ya kufa, kwa Roho wake anayekaa ndani yenu.*

26 Sasa ninatumaini ya kwamba Bwana Yesu ataongeza baraka Zake kwenye kusomwa kwa Maneno haya. Tukiona ya kwamba, Pasaka, nimeupiga muhuri katika moyo wangu mwenyewe kama mkutano ulio mkuu kuliko yote, ama tukio lililo kuu kuliko yote ya mwa—mwaka.

27 Ninataka kuwaomba mniwie radhi kwa dakika moja. Hivi kwa namna fulani hiyo si inatoa sauti kubwa kwenu, kama kunguruma kwa namna fulani? Ni sawa? Mnaweza kuisikia vizuri namna hiyo? Loo! Hamwezi kusikia. Hiyo ni bora zaidi, namna hiyo? Sikutaka kukaribia sana.

28 Sasa, sababu ya mimi kusema jambo hili, ni kwa sababu ya kwamba, Pasaka, Yeye alithibitisha yale Biblia iliyokuwa imesema. Maandiko yote yaliyoandikwa juu Yake kwamba atayatimiza, Yeye alitia Muhuri Umasihi Wake hapo alipofufuka katika wafu, ule Muhuri wa pasaka. Tuna mengi sana ya hiyo siku hizi tunayozungumzia, kwamba, kununua mihuri ya Pasaka. Vema, ninataka kuzungumza asubuhi ya leo juu ya: *Muhuri Wa Pasaka*. Ni muhuri wa tofauti na ule tunaonunua na pesa zetu, kama muhuri wa kugongwa juu ya barua kwa ajili ya, nafikiri, Shirika la Kifua Kikuu ama vyovyote wanavyoliita. Na—nafikiri muhuri huu ni muhuri wa tofauti kidogo. Na kwa kuwa Pasaka ndiyo siku kuu ya mwaka kwetu sisi Wakristo ambao tunadai kwamba tu watoto wa Mungu, ninataka kujaribu kuufafanua tuone jinsi tunavyopaswa kushiriki kitu hiki kikuu ambacho Kristo alitufanyia.

29 Neno la Mungu lilikuwa limenenwa mamia mengi, mengi ya miaka kabla ya Kuja Kwake, juu ya kusulibishwa Kwake,

na juu ya kifo Chake, na mateso Yake, na pia juu ya kufufuka Kwake. Tutakuwa tukizipitia ibada hizi, labda, juma lijalo, tunaposikiliza vipindi vye—vyetu vya redio; na katika makanisa yetu, pamoja na wachungaji wetu, na kadhalika, juma hili lijalo.

30 Lakini kati ya siku zote na mambo yote ambayo Yesu alifanya, na bila shaka tukifurahia madhihirisho Yake yote ya Neno la Mungu na yale aliyotenda kulitimiza: juu ya kuwaponya wagonjwa, kuwafufua wafu, kutoa pepo, kuhubiri Injili kwa maskini, na kutimiza kila Neno ambalo Mungu alisema ya kwamba Yeye angefanya atakapokuja; na halafu pia kuteswa kwa ajili ya dhambi zetu, badala yetu, awe upatanisho kwa ajili ya dhambi, pale msalabani, ambapo hakuna mtu mwingine yeyote angaliweza kufanya jambo hilo ila Yeye. Lakini zaidi ya hayo yote, ninafikiri Pasaka ilitia muhuri jambo hilo lote.

31 Kwa sababu, kulikuwa na manabii duniani, ambao walikuwa wametabiri kabla Yake. Kulikuwa na manabii duniani, ambao walikuwa wamewaponya wagonjwa, hata kuwafufua wafu, na kufanya ishara zile zile alizozifanya Yesu.

32 Lakini Pasaka ilithibitisha jambo hilo. Ilitia Muhuri Neno la Mungu milele, kwa ajili ya mwaminio wa kweli. Majonzi yote na mashaka viliangamizwa, kwenye ile asubuhi yenye baraka. Mwanadamu alikuwa amefungiwa, kama ilivyokuwa, gerezani, hata watu wa kidini kabla ya siku hii, kwa maana walikuwa wameninii . . . wameona miamsho mikuu ya kidini, na matendo ya Roho Mtakatifu, na kadhalika. Lakini wakati mwanadamu alipokufa, ilionekana kana kwamba yote yamekwisha. Bali wakati Huyu alipokuja, na kusema, "Nina nguvu ya kuutoa uhai Wangu; nina nguvu za kuutwaa tena." Na kisha akaenda akathibitisha aliyosema. Kwangu mimi, huo—huo ndio muhuri wa jambo hilo, wakati—wakati jambo fulani linasemwa kisha mtu unageuka na linathibitishwa.

33 Kama mtu alisema, kama Columbus, aliamini dunia ilikuwa ni duara, naye akaangalia meli, kama tunavyoambiwa, jinsi zilivyoingia, naye angeweza kuona mlingoti mapema sana kabla ya kuiona hiyo meli. Na hilo lilimthibitishia ya kwamba dunia ilikuwa ni mviringo. Watu hawakuamini jambo hilo katika siku hizo, bali yeye alikuwa ni mtu anayeona mbali. Alitoka akaenda kuthibitisha kile hasa alichokuwa ameona, kwamba hiyo ilikuwa ni kweli.

34 Na Mungu alikusudia kuthibitisha Neno Lake, ile Kweli. Kwa hiyo Yeye . . . Kulikuwako na Mtu mmoja tu ambaye angeweza kufanya jambo hilo, na huyo alikuwa ni Yesu. Naye alikuja na akathibitisha jambo hilo kuwa ni Kweli. Likalitia muhuri. Na hilo lilivunja mihuri yote ya majonzi, na kutawanya u—ushirikina wote wa dini zingine, na kadhalika, ambapo watu wakuu wameinuka na kusema mambo makuu, ya ajabu; bali wao, kila mmoja wao, yuko kaburini. Bali dini yetu ya Kikristo

ndiyo pekee iliyo na kaburi lililo tupu. Na hilo linanithibitishia ya kwamba Yeye ni Mungu wa wafu, na Mungu wa walio hai, kwamba angeweza kuwafufua wafu, wapate kuishi tena. Nami. . .nguvu hizi za kuhuisha, Roho Wake wa kuhuisha, amethibitisha katika miaka hii yote ya kwamba Yeye Ndiye anayeweza kuwahuisha wafu, wawe hai tena.

35 Na wakati Yeye alipothibitisha kwa ahadi Yake, nguvu hizi kuu za kushinda alizokuwa nazo, kwenye Pasaka Yeye alithibitisha ya kwamba angeweza kushinda mauti, kuzimu, na kaburi. "Mimi ndimi niliyekuwa nimekufa, na niko hai tena, na ninaishi milele na milele; na nina funguo za—za mauti, kuzimu na kaburi." Ni ta—tamshi la namna gani kwa mtu yeyote kutoa. Na si kwamba tu Yeye alilitoa, bali alikuwa tayari amethibitisha ya kwamba Yeye—Yeye alikuwa na kile alichodai kuwa nacho.

36 Nami nafikiri, Mungu na aiharakishe ile siku wakati ambapo sisi, kama Wakristo wanaoiamini Biblia hii, tunaweza kuthibitisha yale tunayozungumzia. Unaona? Hilo ndilo linalofanya, kama ilivyosemwa muda mfupi uliopita, "Chumvi ya dunia," yule dada aliyosema. Hiyo ni kweli. Ulimwengu unaitafuta chumvi hii. Na tunapoweza kuthibitisha kwa maisha yetu, na kwa Biblia, ya kwamba maisha yetu yanathibitisha lile Neno kwamba linaishi siku hizi, ya kwamba hiyo ndiyo ile siku tunayoitazamia.

37 Neno, "Roho huyu . . ." Warumi 8 pale, hicho cha 11, ilisema, "Kama Roho huyu aliyemfufua Yesu Kristo akiwa ndani yenu, Yeye ataihuisha pia na miili yenu iliyo katika hali ya kufa." Si kwamba tu Yeye alimthibitishia Yeye, alituthibitishia sisi, ya kwamba Yeye alikuwa Ndiye Yehova Mkombozi na alikuwa na mamlaka juu ya mauti, kuzimu na kaburi, bali Yeye pia ametupa fursa ya kumkaribia Roho yule yule, ili kwamba sisi nasi tuweze kuwa na uhakika ya kwamba sisi pia tunahuishwa na Roho huyo. Kwa kuwa Roho aliyemfufua Kristo katika wafu anaishi katika mwili wako. Yeye pia atauhuisha na mwili wako ulio katika hali ya kufa. Sasa, neno *kuhuisha* linamaanisha "kufanywa hai baada ya kufa." Baada ya kufa, ndipo utahuishwa.

38 Ulimwengu umefungwa katika shaka, kwa nyakati nyingi hadi kufikia wakati huo. Hili lilithibitishwa, sio tu kuzungumziwa, bali lilithibitishwa. Nafikiri ya kwamba kitu chochote kinachofaa . . .

39 Kama vile Yesu alivyosema, "Basi enendeni, mkawafundishe mataifa yote; na kuwathibitishia, kwa kuwaonyesha nguvu za Mungu. Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio." Hao wanaoahidi na kusema ya kwamba wanaamini, Yeye alitupa ufahamu dhahiri wa hilo, ya kwamba, "Ishara hizi zingefuatana na hao waaminio." Ingekuwa ni thibitisho la ushuhuda wao. Sasa, tunaweza kusema tunaamini. Lakini mpaka tutakapokuwa na ishara iliyothibitishwa ambayo alisema

kwamba ingekuwa juu yetu, basi sisi *tunakiri* tu kwamba ni waaminio, wala si suala la *kumiliki* kwa waaminio.

40 Kwa kuwa, kumbuka, siku chache zilizopita, nilikuwa nikisikiliza kipindi cha re—redio kwenye KAIR huko Tucson. Na huyu mhudumu alikuwa anatupinga, ya kwamba, "Dini ya pentekoste haikuwa chochote ila ni uongo tu. Kulikuwa na . . . Wasiisikilize. Haikuwa thabiti." Kisha akasema, "Mtu yeyote aliyenena kwa lugha, na mambo haya mengine, na kudai kuwa ninii, kuponya wagonjwa, na kadhalika, kwa maombi, ya kwamba mtu ilimpasa kuachana nayo. Na kuwaombea maskini watu hao dhaifu, kwa maana wao walikuwa wako katika hali ya ku—kudanganyika, kwamba walikuwa na kasoro fulani." Loo, jinsi ambavyo ningalipenda kuzungumza na ndugu huyo kwa muda kidogo tu! Naye akasema ya kwamba ninii . . . "Ya kwamba, mambo hayo walipewa tu wale mitume kwenye Siku ya Pentekoste, na hao peke yao."

41 Ninaona ya kwamba, miaka thelathini baadaye, Paulo alikuwa akiweka karama hizi Kanisani. Katika Wakoritho wa Kwanza 15, ya kwamba, "Yeye aliweka Kanisani karama ya kunena kwa lugha, miujiza. Na karama hizi zingine zote ziliwekwa Kanisani."

42 Yesu alisema jambo hilo. "Enendeni ulimwenguni mwote mkahubiri Injili kwa kila kiumbe." Umbali gani? "Ulimwenguni mwote." Kwa nani? "Kila kiumbe." Kamwe hawajaipokea bado. "Na ishara hizi zitafuatana na hao waaminio." Kwa muda gani? "Ulimwenguni mwote." Kwa nani? "Kila kiumbe. Ishara hizi zitafuatana na hao, ulimwenguni mwote, na katika kila kiumbe. Ishara hizi zitafuatana na hao: kwa Jina Langu watatoa pepo; watasema kwa lugha mpya; wakishika kitu cha kufisha, ama nyoka, au kunywa kitu cha kufisha, hakitawadhuru; wataweka mikono yao juu ya wagonjwa, nao watapata afya." Hilo lilikuwa ndilo agizo Lake la mwisho kwa Kanisa, Marko mlango wa 16.

43 Paulo anaweka karama hizi Kanisani, miaka thelathini baadaye. Na akasema, katika Wagalatia 1:8, "Kama Malaika kutoka Mbinguni akiwahubiri ninyi Injili nyingine yoyote mbali na Hii ambayo imepokelewa tayari," unaona, iliyohubiriwa tayari, "na alaaniwe." Ninaamini ya kwamba pentekoste ilianza bila ya kuwa na mwisho. Ninaamini inapaswa kuwa ni kwa kila kiumbe, nyakati zote, mahali pote, kwamba pentekoste inapaswa kudumu daima. Baraka za pentekoste zinapaswa kuwa juu ya watu.

44 Na sasa, baraka hii ya pentekoste ni nini? Ni thibitisho la ufufuo. Si ajabu Injili Yenyewe inamaanisha "habari njema." Habari njema ya kitu gani? Yeye amefufuka katika wafu. "Na kwa kuwa Mimi ni hai, nanyi mtaishi pia." Ninyi ambao mlikuwa mmekufa katika dhambi na maovu, Mungu ametuhuisha pamoja, kwa Roho yule aliyemfufua Yesu katika

wafu. Na sasa tumeketi katika ulimwengu wa Roho pamoja Naye, tukishirikiana Naye, tukizungumza Naye. Ni furaha ya jinsi gani kuwaambia watu hadithi hiyo, wanaoamini kwamba jambo hilo ni Kweli!

45 Ninashangaa, leo. Ni yale yanayotendeka. Je! hivi kweli sisi tunawapeleka watu kwa Mungu, ama tunawapeleka tu kwenye kanisa? Hatuna budi kuwapeleka kwa Kristo, ambako kuna nguvu hizi za kuhuisha. Ni vizuri kwenda kanisani. Hakika. Kama huo ndio umbali tunaofikia, si umbali wa kutosha. Unapokuja kanisani, hilo ni jambo zuri; bali nenda hadi kwa Kristo, unapotoka kanisani, kwa kuwa hatuna budi kupokea nguvu hizi za kuhuisha, ikiwa tunatarajia kuwa kwenye ule ufufuo wa watu wote, kwa sababu ndicho kitu pekee kitakachotufufua kutoka kwa wafu. "Kwa kuwa ikiwa Roho huyu aliyemfufua Yesu toka kwa wafu anakaa ndani yenu, pia ataihuisha, ataifanya, ataifufua miili yenu iliyo katika hali ya kufa." Ni ahadi ya jinsi gani kwetu!

46 Sasa angalia. Kiini chenyewe cha ufufuo huu ni kupiga mbiu na kuonyesha, na kuthibitisha ya kwamba Yesu amefufuka katika wafu. Si mfu. Yu hai. Anaishi hapa. Yumo ndani yetu. "Nitakuwa pamoja nanyi, hata ndani yenu. Bado kitambo kidogo na ulimwengu hautaniona tena. Hata hivyo, ninyi mtaniona, kwa kuwa nitakuwa pamoja nanyi, hata ndani yenu, hadi ukamilifu wa dahari."

47 Sasa, kama Wakristo, sote tunadai Yeye yu hai, ama tumehuishwa kutoka—kuhuishwa kutoka katika maisha... kutoka mautini kuingia Uzimani, kwa Roho Wake. Na kama hatujahuishwa, basi hatujafanywa hai.

48 Sasa tutaliingilia somo hili, Bwana akipenda, na kwa namna fulani tulifundishe kwa dakika chache, jinsi ambavyo: je! tumehuishwa, na je! tunaweza kuwa na hakika ya kwamba hii ni Kweli?

49 Sasa, haya ni maisha yako mwenyewe, haya ni maisha yangu. Ni pale ambapo ninii...Kama hii si Kweli, yale ninayotaka kusema, basi mimi ni mmoja wa watu walio wapumbavu kabisa ulimwenguni. Nimeyatoa maisha yangu kwa kitu ambacho hakifai kitu, na wewe vivyo hivyo. Bali kama ni Kweli, basi ninawiwa kila kitu nilicho. Ninawiwa kila kitu ambacho ningeweza kuwa, kwa huduma hii, ambayo tunaitetea. Na ninafikiri ya kwamba haitupasi kupoteza shauku yetu.

50 Na tunapoona Pasaka ikikaribia, inafanya tu kitu fulani ndani yangu, kwa kuwa ni—ninajua hiyo ndiyo siku ambayo kitu hicho kilitiwa muhuri milele, machoni pa Mungu.

51 Sasa, tunaona, ni Roho yeye yule aliyemfufua Yeye kutoka kaburini, ambaye anaishi ndani yetu. Sasa, jambo hilo lingewezekanaje? Roho aliyemfufua, Mungu, Yesu katika wafu, ana makazi ndani yetu.

52 Sasa, sasa, Roho ndiye anayehuisha. Neno silo linalohuisha. Roho ndiye anayehuisha Neno, ama anayelipa Neno Uhai, anayelipa mabawa lipate kuruka, anayelipa fursa ya kukaribia. Roho ndiye anayefanya hivyo.

53 Sasa, ngano, peke yake, ni ngano tu; bali wakati ule uhai wa kuhuisha unapoingia ndani yake, katika hiyo ngano, ndipo unaipa uhai. Nasi ambao tulikuwa wafu wakati mmoja, tulioumbwa katika sura ya Mungu, na hata hivyo tumekufa katika dhambi na makosa, kuna njia ambayo Mungu alikuwa nayo kuutia Uhai huu unaohuisha ndani ya miili yenu iliyo katika hali ya kufa. Ninazungumza juu ya mwili wako.

54 Sasa, Yesu alikuwa ndiye lile Neno. Mnaamini jambo hilo, sivyo? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] "Hapo mwanzo . . . " Yohana Mtakatifu 1, "Hapo mwanzo kulikuwako Neno, Neno alikuwako kwa Mungu, Naye Neno alikuwa Mungu. Naye Neno alifanyika mwili akakaa kwetu."

55 Sasa, kama Masihi aliyeahidiwa, Yeye alihuisha kila Neno lililotabiriwa kwamba angelifanya; kuponya wagonjwa, na jinsi ambavyo angezaliwa na bikira, yote hayo, aliyatimiza. Ni kweli. Yeye alikuwa ndiye lile Neno, lililodhihirishwa hapa duniani, bali hangeweza kufanya jambo hili kama Mwanadamu tu. Ilihitaji Roho wa Mungu, aliyeishi ndani Yake, kuzihuisha ahadi hizi Kwake. Natumaini tunapata jambo hili dhahiri sana sasa. Yesu, akiwa ni Mwanadamu, Mwenyewe, ule mwili, bali ilihitaji Roho aliyekuwa ndani Yake, yule Roho. "Si Mimi ninayefanya kazi hizi. Ni Baba Yangu anayeishi ndani Yangu. Yeye ndiye anayefanya kazi hizi." Unaona? Yesu Mwenyewe alikuwa ni Neno, kwa sababu alikuwa. Kabla Mungu . . .

56 Hili ni neno baya la kutumia, nami ninatumaini mtalichukua vizuri, mbele ya umati. Bali Yeye alichaguliwa tangu zamani kwa kujua tangu zamani kwa Mungu, jinsi ambavyo mpango wa Mungu ungekuwa, ya kwamba Yeye angemtuma Mkombozi, na Mkombozi huyu angeweza tu kuwa ni Mwanawe Mwenyewe. Kwa hiyo, basi, hiyo ilikuwa ni ahadi ya Mungu, kote tangu kwenye bustani ya Edeni, ya kwamba Yesu angekuwa hapa. Hapa Yeye alikuwa Mwanadamu, aliyezaliwa na bikira, bali ilihitaji Roho wa Mungu kulihuisha Neno hilo Kwake. Naye alikuwa ni Neno, lililohuishwa, Neno lililohuishwa kwa wakati ule. Wakati ulikuwa umewadia ambapo ilikubidi kuwa na Mkombozi. Torati ilikuwa imeshindwa. Mambo mengine yalikuwa yameshindwa. Sasa, inahitaji Mkombozi, Naye alikuwa ndiye huyo Mkombozi aliyeahidiwa. Yeye alihuishwa na Neno la Mungu.

57 Na sasa kama Roho yeye yule aliyekuwa juu Yake apate kuwa Mkombozi katika wakati ule, ambaye tumekubali sasa ahadi Yake katika siku hizi za mwisho, kile ambacho kingetukia; kama wewe ukiwa sehemu ya hilo Neno, umekombolewa pamoja Naye,

kwa maana Roho yeye yule aliyeishi katika Kristo anaishi ndani yako, akiyahuisha maisha yako kwa ajili ya wakati huu. Na ataninii pia, katika wakati wa mwisho, ataihuisha miili yenu iliyo katika hali ya kufa, aifufue, aiinue tena. Hilo linaondoa majonzi tunapoliangalia, katika hilo. Na hiyo ni Kweli. Unaona?

58 Warumi hapa, Paulo ametuthibitishia hilo. Mnaona? "Ikiwa Roho aliyemfufua Yesu katika wafu anakaa ndani yenu, yeye pia ataihuisha na miili yenu iliyo katika hali ya kufa." Huyu ni Roho yeye yule aliyemfufua, aliyemhuisha mwaminio wa kweli apate Uzima wa Milele. Roho aliyemfufua Kristo katika wafu huishi ndani ya mwaminio, anamhuisha mwaminio apate Uzima wa Milele.

59 Kuna Uzima mmoja tu, Roho mmoja wa Milele, Uzima mmoja wa Milele, na huo ni Mungu. Mungu, peke yake, ndiye wa Milele. Na halafu sisi, tukiwa ni watoto Wake, tu sehemu Yake, hiyo ni kusema, sifa za mawazo Yake. Nalo wazo linatamkwa na linakuwa neno. Ndipo, kila mtu binafsi hapa ndani, aliye na Uzima huu wa Milele, alikuwako kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu, katika mawazo ya Mungu. Ndiyo njia pekee ingaliweza kuwa, kwa maana wewe ni sifa. Hilo ni tamko la wazo, limekuwa Neno; na Neno limepata Uzima, na ni la Milele. Hiyo ndiyo sababu tuna Uzima wa Milele. Kwa kanuni ile ile ambayo yule Mwana mkuu wa Mungu, yule Mkombozi; tunakuwa wana na binti za Mungu, kupitia kwa Roho yule yule, kwa kutangulia kujua kule kule kwa Mungu.

60 Angalia mamilioni hapa duniani ambao hawakulipokea wakati Yesu alipokuwa hapa. Lakini jinsi tunavyopaswa kuwa na shukrani asubuhi ya leo, kujua ya kwamba tuna ushuhuda wa moja kwa moja na mathibitisho ya Biblia, ya kwamba tumehesabiwa katika ile asubuhi kuu ya ufufuo unaokuja, ile Pasaka kuu. Tuna arabuni yake, sasa hivi katika miili yetu iliyo katika hali ya kufa. Wale waliochaguliwa tangu zamani ndio wa kwanza, bila shaka, kuhuishwa, wakati Roho Mtakatifu atakapokuja kudai walio Wake.

61 Sasa, hilo hapo tamshi kubwa, na ninawataka ndugu zangu wahudumu wajaribu kufahamu jambo hili. Unaona? Hapo mwanzo, Mungu, yule Roho mkuu, Yeye hata hakuwa ni "Mungu" wakati huo. Alikuwa ni yule Wa Milele. *Mungu* ni "kitu cha kuabudiwa." Hakuwa na kitu cha kumwabudu. Hakukuwako na—hakukuwako na Malaika, hakukuwako na kitu chochote. Ni Mungu peke yake, Yeye peke yake, ni wa Milele. Lakini, kusudi awe Mungu, ilibidi pawepo na kitu cha kumwabudu, kwa hiyo Yeye akawaumba Malaika, na Viumbe, na Makerubi, na kadhalika, wapate kumwabudu. Mpango Wake mkuu ukaanza kujikunjua.

62 Lakini kumbuka, wewe, katika ki—kimo ulicho, asubuhi hii, kama hukuwa katika mawazo Yake wakati huo, huko sasa. Kwa

kuwa wewe, kuna sehemu fulani iliyo ndani yako, ambayo ni ya Milele, na Milele ni ya Mungu peke yake. Na katika Mungu kulikuwako na mawazo Yake ya wewe ukiwa umeketi papo hapo unapoketi sasa. Katika mawazo Yake, nilisimama mimbarani asubuhi ya leo, kwa maana Yeye hana kikomo na anajua mambo yote. Kwa hiyo Yeye angeweza kujua mwisho tangu mwanzo, kwa kuwa Yeye ni wa Milele. Na wewe, ukiwa ni Mwana wa Mungu ama binti wa Mungu, basi ulikuwa katika mawazo Yake hapo mwanzo.

63 Na ndipo wakati Roho Mtakatifu alipokuja, nawe uko duniani, ukitembea hapa kama mwenye dhambi, ndani kabisa maishani mwako kuna kitu fulani. Hujui kinachotendeka, bali una njaa. Nilimsikia ndugu Mpresbiteri; nilimsikia M—Mbaptisti akizungumza juu ya jambo hilo, kule nyuma, alikuwa ni M—Mbaptisti Mawazo Huru, akihubiri mahali anapoweza kuhubiri. Ndugu mwenzangu, kwamba wewe, kuna kitu fulani ndani yako, kitu fulani ambacho hukukiweka humo ndani. Ni kitu fulani ambacho hungeweza kutamani kiwe humo ndani. Ni kitu ambacho ni kinyume na tabia asilia yako mwenyewe. Ni kujua kwa Mungu tangu zamani, kukitukia, Neno la Mungu.

64 Na Yesu alizaliwa Mwana wa Mungu, apate kuwa Imanueli, dhihirisho kamili la Mungu ndani ya Mwanadamu. Naye alimwona katika utii mkamilifu, kule kwenye Mto Yordani, akibatizwa na yule nabii. Na mara alipomtii, na akatembea kutoka majini, Mbingu zilimfungukia Yohana. Naye akamwona Roho Mtakatifu akishuka kutoka Mbinguni, akisema, "Huyu ni Mwanangu mpendwa." Unaona? Utii mkamilifu, Roho alikuwa amemtafuta, katika utii.

65 Loo, ewe mwanamume ama mwanamke mkaidi, asubuhi ya leo, wakati unapoketi hapa, na kuna kitu fulani ndani yako kinachokwambia Hili ni kweli, ni Roho Mtakatifu akikutafuta, kukuleta kwenye maarifa ya Kweli ya wakati huu tunaoishi sasa, si wakati fulani uliopita, wakati huu wa sasa.

66 Kulikuwa na maelfu pale waliokuwa wakitii wakati uliopita. Bali palikuwapo na wakati wa saa ya sasa, huo ulikuwa ndio wakati ambao Yesu alikuwa atokee, na hapo lilisimama Neno. Hapo walisimama watu. Na hapa palikuwapo na dhihirisho la Mungu likitukia, kuthibitisha ya kwamba hiyo ilikuwa ni Kweli.

67 Na kama Wapentekoste, siku hizi, hebu niseme jambo hili, ya kwamba tunasimama katika siku hizi za mwisho ambapo Mungu aliahidi angemmwaga Roho Wake juu ya wote wenye mwili, na wanawe na binti Zake wangetabiri. Kwa kuwa Yeye alisema, "Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio." Wakati huo umewadia. Hilo ndilo linaloufanya huo uumbaji ndani yako.

68 Kama nilivyosema hapa, si muda mrefu uliopita, lilisikika la kukufuru kidogo; bali natumaini halisikiki hivyo, kwenu, asubuhi ya leo. Yule mkulima aliyemwekea tai, ama

aliyemwekea kuku, naye alikuwa na yai la tai. Wengi wenu mnakumbuka hadithi hiyo ya maskini yule tai akizaa nanii—huyu nanii. . . Ama, yule kuku akimzaa huyu kifaranga hapa, ama—ama—ama yai la tai chini ya manyoya yake ya kuku. Unaona? Ni suala la mazingira.

69 Kanisa la Presbiteri, kanisa la Methodisti, kanisa la Baptisti, lolote la hayo linaweza kuangua tai hawa. Hakika. Mazingira ndiyo yanayolisababisha. Kama vile Dk. Bosworth alivyozoea kusema, "Ungeweza kuchukua yai la kuku na kuliweka huku, chini ya kitoto cha mbwa, na umfunge, kitoto hicho cha mbwa kingeangua kuku." Kwa nini? Ni suala la mazingira. Na wakati kanisa lolote ama kundi lolote ambalo litakusanyika pamoja, na kuomba mpaka watupilie mbali kanuni zao za imani na kadhalika, na kuangalia moja kwa moja usoni mwa Mungu, litaangua tai kwa hakika tu kama ninavyosimama hapa.

70 Hilo ndilo ambalo ninafikiria kwamba kundi hili la wafanyabiashara limefanya, kujaribu kuvunja mazingira. Tunagawanyika makundi-makundi sana. Mmoja ni mfuasi wa *hili* na *lile*. Hebu na tuvunje mazingira na tuingie kwenye mazingira ya ibada ya Kimbinguni. Tuweke mazingira sahihi, tai watazaliwa, na—na kutoka kwenye kanisa lolote, mahali popote.

71 Basi tai huyu mdogo alitembea pamoja na kuku huyu kwa muda mrefu, lakini kwa namna fulani ule m—mlio ulikuwa ni wa kigeni. Hakuelewa yale kuku aliyomaanisha wakati alipokwaruza kwenye lu—lu—lundo la mbolea katika vi—vitalu. Na hicho hakikuwa ni chakula, kwake. Naye alikula wadudu, na kadhalika, ambao tai hali. Kwa hiyo lilionekana ni jambo la kigeni, lote, kwake. Naye alikuwa ni mtoto wa bata mwenye sura mbaya, alikuwa hivyo. Sisemi jambo hili kwa kukufuru. Labda alikuwa ni Mbaptisti Mwenye Mawazo Huru, na, lakini ni kitu kama hicho, ama Mpresbiteri.

72 Lakini, mwajua, siku moja mama yake alijua ya kwamba alikuwa ametaga yai. Lazima kuweko na mtoto mahali fulani. Kwa hiyo akatupa mbawa zake kubwa kwenye upepo, naye akatafuta na kutafuta, akilia kwa sauti yake yote. Basi siku moja, alipitia juu ya kile kitalu. Na wakati maskini tai huyu mdogo aliposikia mlio huu alioufahamu, hajawahi kamwe kuusikia hapo kabla, bali alitambua ya kwamba ulimwenea kama glavu iliyovaliwa mkononi. Naye akajua ya kwamba huyo alikuwa ni mama yake. Mama akajua huyo alikuwa ni mwanawe. Alikuwa akimtafuta.

73 Vivyo hivyo na Mungu pia, katika kila wakati, amelichagua Kanisa Lake kwa ajili ya wakati huo, Ujumbe kwa ajili ya wakati huo. Nao wangeweza kuwa na torati na kitu chochote wanachotaka. Lakini wakati hiyo saa inapofika, Roho Mtakatifu wa Mungu, ambaye hapo mwanzo aliwaziwa na kunenwa kwa

ajili ya wakati huo, Roho huyo hulitafuta hilo yai. Na wakati anapousikia huo Ujumbe, hakuna kanisa la kimadhehebu litakalozuia jambo hilo. Atainuka apande kwenye viwango vya juu sana. Hana budi kufanya hivyo. Ni ndege wa tofauti. Ni kiumbe cha tofauti. Yeye ni tai, naye atasikia huo mlio. "Kondoo Wangu huisikia Sauti Yangu."

Kama vile mtu fulani alivyosema, Ndugu Williams, "Chakula cha Kondoo."

74 "Kondoo Wangu huisikia Sauti Yangu. Mgeni hawatamfuata." Haidhuru kanisa limekuwa aminifu jinsi gani, na kwamba lina jina kubwa jinsi gani. "Wakati kondoo Wangu wanapoisikia Sauti Yangu," ambayo ni Neno, "mgeni hawatamfuata." Wataenda moja kwa moja kwenye hilo Neno, na wanaweza kufanya hivyo. Ni kama su—su—sumaku.

75 Siku moja, huko Indiana, nilikuwa nikizuru vinu vya feleji, na filimbi ikapigwa. Na wote wakavua aproni zao, na kuanza kufagia ninii. . . kutoka kwenye kerezo zao, kuzipeleka katikati ya sakafu, zile takataka za vyuma walivyokuwa wamefua siku nzima. Nami nilikuwa nikitembea pamoja na mtu aliyekuwa akinitembeza, ndipo akasema, "Hebu angalia jambo hili." Na kwa hiyo kila mtu akaweka nguo ya—yake ya benchi me—mezani, akaondoka.

76 Huko nyuma nyuma kabisa, akabonyeza kitufe kidogo. Ndipo sumaku kubwa ikapitia pale, na ikachukua kila kipande cha chuma hicho kilichokuwa kimekatwa kutoka kwenye vipande hivyo, sasa, kisha ikaondoka. Ikaondoa nguvu zake za sumaku; ikaviangusha kwenye kuba. Ndipo vikayeyushwa tena, kwa ajili ya kipande kingine cha—cha bidhaa, kitu kile kile, ekseli ama chochote kile walichokuwa wakijenga.

77 Nami nikasimama pale na kuangalia jambo hilo, mpaka ni—nikajisahau. Basi nikasema, "Ninashangaa jambo fulani."

Akasema, "Ni kitu gani, bwana?"

Ndipo nikasema, "Ninaona ya kwamba baadhi ya hivyo havikuinuliwa juu."

78 Akasema, "Ni alumini, na sumaku haiwezi kuinua alumini."

79 Nikasema, "Kumbe." Na akasema. . . Kisha nikasema, "Vema, unaona, kile *pale* kipande cha chuma kimekaa pale."

"Lakini, unaona, bwana, kilikuwa kimekaziwa chini kwa bolti."

80 Nikasema, "Kumbe." Na wakati alipokitoa, nilisema, "Sasa ni jambo gani litakalotukia, kile *pale* nje?"

81 Akasema, "Kinarudi moja kwa moja kwenye kinu, kinamiminwa kwenye kuba, na kinarudi moja kwa moja na kufanya gurudumu lingine."

Nikasema, "Bwana asifiwe!" Jambo ndilo hilo. Unaona?

82 Kuna sumaku kuu iliyoko mbinguni, ambayo Mungu siku moja ataigusa kwa vidole Vyake. Hakuna mtu anayejua wakati Yeye atakapokuja, si hata Malaika wa Mbinguni, hawajui. Mungu pekee ndiye anayejua. Bali kumekuwako na vipande ambavyo vimekatwa toka kwenye Biblia, Wakristo wa Biblia, waaminio wa wakati huu. Mmoja wao huenda alikuwa ni ekseli huko nyuma katika siku nyingine. *Huyu* anaweza akawa ni sehemu nyingine. Atafanya mfumo mkuu wa Mungu. Bali watafinyangwa kwenye nyungu ya kuba kubwa ya Mungu, na kumiminwa tena wawe sura za Mungu. Na ni wale tu waliotiwa sumaku kwake ndio watakaotwaliwa juu. Loo, jinsi ya kuninii . . . Ni majaliwa ya jinsi gani, kujua ya kwamba kuna jambo fulani katika ufufuo linalofungamana na sisi!

83 Sasa, angalia, tambua wito wa Neno la Mungu, ambalo ni sehemu yake. Na ni tai kwa tai. Sasa, kama huyo mama angalilia kama mwe—mwewe, yeye asingaliifahamu kamwe. Ingekuwa ni afadhali angeendelea tu aishi kwenye kile kitalu. Lakini ulikuwa ni ule mlio wa tai. Kulikuwa na kitu fulani kilichokuwa ndani ya maskini jamaa huyo, ambacho kilimfanya ajue kwamba yeye alikuwa ni tai.

84 Na jambo lile lile lina kila mwaminio wa kweli. Wakati kuhubiriwa kwa Neno la Mungu kunapotokea, na kunathibitishwa na kuhakikishwa ya kwamba ni Neno la Mungu kwa ajili ya wakati huu, basi kuna kitu Fulani ndani ya mwaminio huyo. Sijali baba yake alikuwa ni mwaminifu jinsi gani kwa kanisa, ama jinsi mama yake alivyokuwa mwaminifu, ama babu zake, na kama kanisa hilo linafundisha kinyume na wakati huu wa Ujumbe wa ubatizo wa Roho Mtakatifu. Kuna kitu fulani ndani Yake kinachopaza sauti. Yeye ataondoka kwenye kitalu hicho. Hana budi kuondoka. Kuku huenda walikuwa sawa siku moja, bali haya ni majira ya tai. Unaona? Ni—ni tofauti. Kuna kitu fulani, ambacho, hana budi kuondoka kwenye tundu hilo la kale na kuruka aingie angani. Ndipo mwili huu wa duniani unahuishwa na kuletwa, na Roho anayehuisha, apate kulitii Neno la Mungu.

85 Sasa, wakati huyu Roho Mtakatifu, anayewakilishwa kama tai arukaye juu ya nchi, na kumpata mwaminio. "Hakuna mtu awezaye kuja Kwangu, hakuna mtu awezaye kuja Kwangu anavyotaka. Wote alionipa Baba watakuja Kwangu, bali hakuna mtu anayeweza kuja kwa nafsi yake mwenyewe." Si mawazo yako mwenyewe, kuvuta kwako. Ni Mungu, akivuta. Unaona? "Wote alionipa Baba watakuja Kwangu."

86 Sasa, Roho Mtakatifu yupo hapa duniani, akiwatafuta hao watu ambao Mungu amewakusudia Uzima katika wakati huu. Na mara tu anapowapata, anafanya kama tu alivyofanya kwa Yesu Kristo, yule Mwana kipeo kikuu kabisa cha Mungu Ambaye alitukomboa sisi sote. Anashuka na kupachukua mahali Pake pa kukaa katika maisha ya mwanadamu, sasa, angalia, alileta

nguvu za kuhuisha. Sasa, nguvu hizo za kuhuisha zilizomjia Yesu zilimhuisha apate kudhihirisha kila ahadi ya Neno la siku hiyo. Vivyo hivyo na Roho Mtakatifu anayekuja juu yetu katika siku hii, kama si roho mtakatifu wa dhihaka, kwamba wewe si Ibilisi akimdhihaki Roho Mtakatifu, bali ni Roho Mtakatifu halisi, wa kweli. Atadhihirisha ahadi ya wakati huu.

87 Wakati aliposhuka juu ya Luther, alidhihirisha ahadi ya wakati huo. Wakati aliposhuka juu ya Wesley, alidhihirisha ahadi ya wakati huo. Wakati anaposhuka katika siku hii, anadhihirisha ahadi ya saa hii. Wakati aliposhuka juu ya Musa, alidhihirisha ahadi ya saa ile. Aliposhuka juu ya Nuhu, anadhihirisha ahadi ya saa ile. Wakati alipoanguka juu ya Yesu, alidhihirisha ahadi ya saa ile. Unaona?

88 Ni Roho Mtakatifu akishuka, kuhuisha, kuwafanya hai wale watu waliochaguliwa na Mungu tangu awali kuwa katika ule Unyakuo. Angalia. Hiyo ni kusema, kama yeye ni tai wa kweli, ataufahamu Ujumbe wa wakati huu kama yeye ni tai wa kweli. Sasa, maskini kifaranga huyo wa tai labda, huko kwenye kitalu, alikuwa akila vema, bali a—alijua haikuwa ni sawa hasa. Lakini basi wakati alipoisikia ile Kweli, ndipo akaipokea Kweli hii. Sasa, katika Yohana 14 . . .

89 Yohana 5:24, hasa, Yesu alisema, akisema hivi, "Yeye ayasikiaye Maneno Yangu, na kumwamini Yeye aliyenipeleka, yuna Uzima wa milele, wala hataingia hukumuni, bali amepita kutoka mautini kuingia Uzimani." Wazia tu jinsi hilo lilivyo rahisi, "Yeye aaminiye." Sasa, namna sahihi ya kusema jambo hilo, "Yeye atambuaye."

90 Sasa, hebu toka uende hapa nje mtaani na umwambie kahaba huyu, "Je! unaamini?"

"Hakika."

"Unaamini Yeye ni Mwana wa Mungu?"

"Bila shaka."

"Umebatizwa?"

"Hakika."

91 Shuka uende kwa mlevi, useme, "Unasikia Hilo? Unamsikia mhubiri huyo akihubiri?"

"Naam."

"Unaamini jambo Hilo?"

"Hakika." Unaona?

92 Lakini, "Yeye atambuaye, yeye anayejua mahali pake katika wakati huu, yeye alisikiaye Neno Langu na kumwamini Yeye aliyenipeleka, yuna" (wakati wa sasa) "Uzima wa Milele. Hataingia Hukumuni, bali tayari amepita toka mautini akaingia Uzimani." Ndipo wakati Uzima huu mpya wa Milele unapokaa ndani yako, Hiyo ni dhamana, ama ni arabuni ya wewe

kuhuishwa kutoka katika mwili huu ulio katika hali ya kufa kuingia katika mwili usiopatikana na mauti.

93 Hebu niliseme jambo hilo tena. Wakati Roho Huyu amekupata, wewe mtu binafsi, na amekuja juu yako, Yeye ni dhamana ya urithi wako wa Milele ambao Mungu alikuwazia na kukufanyia kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu. Hiyo ni arbuni yako.

94 Ni kama vile ambavyo ungeniomba nikupe mwaloni, na nikupe mbegu ya mwaloni. Sasa, ma—ma—maisha ya mwaloni yako ndani ya mbegu ya mwaloni sasa, bali inakubidi kungoja mpaka itakapokua.

95 Vivyo hivyo na sisi. Unapompokea Roho Mtakatifu wa Mungu, ni uwezekano wa Mungu unaokungojea, ambao umekutambua tayari. Nawe umetiwa muhuri na Roho wa ahadi, wa Mungu, ukaingizwa katika Mwili wa Kristo. Wakati Mungu alipoangalia chini pale Kalvari na kumwona Yesu akifa, Yeye hakuninii tu...Loo! Alikufa kwa ajili ya Bibi-arusi Wake, ule Mwili, ambao ni Kanisa Neno, Kanisa linaloamini Neno la Mungu la wakati huo, kama ni miguu, mwili, kichwa, ama popote pale palipo. Unaona? Ni...Kristo alikuwa akitokwa na damu na anakufa. Na Mungu, alipokuwa akimwangalia, aliona ufufuo Wake, nalo Kanisa lilifufuka pamoja Naye wakati wa Pasaka.

96 Sasa, ninataka mpate haya yote kwa pamoja, maana nina jambo fulani hapa punde si punde, ninalotaka kusema, Bwana akipenda.

97 Sasa angalieni. Ni arbuni, au ni uwezekano, zile nguvu za kuhuisha za kufufuka kwako, wakati unapompokea Roho Mtakatifu. Sasa anakaa ndani yako, ule uwezekano wake.

98 Angalia, sasa u—uko safarini, ukikua kufikia ufufuo mkamilifu. Hakuna mti unaokua kwa usiku mmoja. Hauna budi kukua, kama tunavyokua katika neema na maarifa ya Mungu. Unabatizwa katika Roho Mtakatifu. Sasa, kama vile Kanisa la pentekoste, lilivyobatizwa katika Roho Mtakatifu, lilianza kukua. Matawi yamekufa. Walikuwa wakiyapogoa. Bali Mti huo ungali unakua, ungali unaendelea, kwa sababu hauna budi kufikia ule ufufuo.

99 Wao wanaongozwa na Roho, kulihuisha Neno kwenu ninyi ambao ni waaminio. Neno linaendelea kuhuisha, unapofikia kwenye tawi la kwanza, tawi la pili, tawi la tatu, na kuendelea kwenda juu. Anaendelea tu kuhuisha. Roho wa Mungu anaendelea kuhuisha kwako.

100 Angalia jambo hilo, Pentekoste, miili yao ilihuishwa na Uzima mpya walioupokea. Hilo linanifanya nijisikie wa kubarikiwa. Wazia. Sasa, hawa hapa watu, wavuvi, watoza ushuru, maskini wanawake wanyenyekevu wa...na wake wa kawaida tu wa nyumbani, maskini wasichana wadogo mabikira.

Walikuwa ni waaminio. Walikuwa wakiamini ya kwamba jambo hili lilikuwa ni Kweli. Waliamini jambo hilo, wakati Yesu alipokufa. Walimwamini Yeye. Na akafufuka tena, katika wafu; waliamini huo kwamba ni ushuhuda wa kweli wa Mungu, ya kwamba alikuwa amemhuisha akawa hai.

101 Sasa, wanaelekea, kwenye ile Siku ya Pentekoste, wapate kupokea hatimiliki-hakiki yao. Je! mnajua hatimiliki-hakiki ni kitu gani? Ni wakati hatimiliki imetolewa. Wao walipanda wakaenda kule juu kupokea hatimiliki yao hakiki. Nao wakahuishwa, ama kweli ni msisimko wa jinsi gani! Walikuwa wamenunua shamba; lilikuwa limenunuliwa kwa ajili yao. Walikuwa wameipokea.

102 Hiyo ni kweli au la? "Tulimwona akifufuka, lakini sasa na vipi kuhusu sisi? Sisi ni mashahidi. Tulisimama tukamwona Mtu huyo akisulibishwa. Tuliona mawingu yakiifunika nchi na kutia mbingu giza. Na ninii—nchi ilitetemeka na kutikisika; ilishikwa na ugonjwa wa wasiwasi. Ndipo wakati. . . Wakamweka kaburini. Wakamchoma mkuki moyoni, kwa mkuki, kisha wakaushusha mwili Wake na kuulaza kwenye kaburi la Yusufu wa Arimathaya."

103 Na ndipo wakaona, ya kwamba, kwenye siku ya tatu, Yeye alifufuka tena. Na kama vile mwanafunzi alivyosema, "Sisi ni mashahidi wa jambo hili. Tulimwona akifufuka. Tunajua yeye yu hai."

104 Sasa jambo hilo lilifanya nini? Hilo liliondoa woga wote. Si ajabu Yesu alisema, "Msiogope. Mimi Ndimi niliyekuwa nimekufa, nami ni hai milele na milele." Unaona? Liliondoa hofu yote, walipofanya jambo hilo.

105 Sasa, lakini walipopanda wakaenda Pentekoste, hapo walipokea nguvu za kuhuisha, zile nguvu zilizowafanya hai.

106 Sasa hapo ndipo ninapofikiri ya kwamba, ninyi ndugu wa Kipresbiteri na wa Methodisti, mnapokea kwa nguvu zisizodhihirika hapo mnapomwamini Bwana Yesu Kristo, bali ile hatimiliki hakiki haijaja bado. Huko ni kule kuondolewa madai kwa hati yake.

107 Mungu alimpa Ibrahimu ahadi. Ibrahimu alimwamini Mungu, na akahesabiwa kwamba ana haki. Bali alitia muhuri agano hilo kwa muhuri wa tohara.

108 Na Mungu hukupa ahadi fulani, kwa uwezekano, ya kwamba utaipokea, na utafufuliwa, mwili huu utatukuzwa pamoja na Yeye wakati wa mwisho. Lakini, unaona, huna budi kupata idhini kwenye hati hiyo ya umilikaji. Na huko kupatiwa idhini ni wakati kila kitu inachodaiwa kimeondolewa, nawe umepata hatimiliki yake hakiki. Una muhuri. Ni yako. Kila kitu kilicho juu yake ni chako. Amina.

109 Na wakati tunapomwamini Yesu Kristo kuwa Mwokozi wetu, na kutubu na kubatizwa, na tunakuja kumwamini Yeye; Mungu hutambua toba yetu na imani yetu Kwake, ndipo anatuma hatimiliki hakiki. Na hatimiliki hakiki ni hakikisho. Ni hakikisho ya kwamba, kila kitu kilichokuwa dhidi yako, umetubu kwelikweli. Haleluya! Na mali hiyo imenunuliwa, nawe una ile hatimiliki hakiki kwa ajili ya thibitisho.

110 Hebu mtu na ajaribu kukuondoa kwenye shamba hilo, aseme ni lake, nawe una ile hatimiliki hakiki mkononi mwako. Hebu na ajaribu kufanya jambo hilo. Hakuna sheria nchini inayoweza kufanya hivyo, kwa maana wewe una ile hatimiliki hakiki.

111 Na hakuna pepo, wala kanisa, wala theolojia yoyote, inayoweza kuvuka mipaka ya thibitisho la Mungu na hatimiliki hakiki, kwamba ubatizo wa Roho Mtakatifu umetukubali katika Yesu Kristo. Sisi tuna hakika tu ya kufufuka kama Yeye alivyofufuka, kwa maana kwa uwezekano tumefufuka katika Yeye tayari. Amina.

112 Mambo ya kale. Yanaifanyia nini miili yetu iliyo katika hali ya kufa? Inabadilisha mawazo yetu, inabadilisha nia zetu. Inaweka shauku zetu kwenye mambo yaliyo huko Juu. Na kuvuta sigara, kunywa pombe, kucheza kamari, mambo uliyokuwa ukifanya, yamekufa. Yako chini yako.

113 Nawe umehuishwa. Na nguvu hizi za kuhuisha zinaufikisha mwili wako kwenye hali ya kunyakuliwa, tayari. Angalia Wapentekoste kule juu, wakati walipohuishwa na Roho Mtakatifu. Nisikilizeni. Wakati hilo kundi la pentekoste kule juu, kwenye ile Siku ya Pentekoste, walipoipokea hatimiliki hakiki kutoka kwa Mungu, hakika, ilizifurahisha nafsi zao. Wakapiga makelele. Waliona ndimi za Moto zimegawanyika juu ya kila mmoja wao. Na jambo hilo liliihuisha miili yao sana, hata wasingeweza kunena katika lugha ya duniani tena. Ilihuisha mwili wao ukanena lugha ya Mbinguni, Mahali wanakokwenda. Nguvu za kuhuisha za Mungu ziliitikisa sana miili yao iliyo katika hali ya kufa, mpaka lugha yao yote ya kibinadamu ikabadilishwa, ikageuzwa ikawa lugha isiyopatikana na mauti. Ni nguvu za kuhuisha za jinsi gani! Ati nini? Kitu cha mwenyewe.

114 "Kama Roho aliyemfufua Yesu katika wafu, akiishi katika miili yenu iliyo katika hali ya kufa, Yeye ataihuisha pia na milii yenu iliyo katika hali ya kufa." Tunahuishwa basi na nguvu za Mungu aliye hai.

115 Ndimi, zilihuishwa kunena kwa lugha ya Mbinguni, kuwazungumzia; kunyakuliwa, kuinuliwa na kuingizwa katika mazingira fulani ya tofauti mbali na yale waliyokuwa wameishi ndani yake. Pia, wakiwa na ule Uzima mpya wa kuhuisha kwao, ulioingia ndani yao, uliihuisha lugha yao. Walinena kwa lugha mpya. Loo, naam!

116 Sasa hebu waangalie. Ilikusudiwa kuwapa, baada ya hii hatimiliki hakiki, ilikusudiwa kuwapa kila ahadi iliyokuwako kwenye hiyo nchi. Kila ahadi iliyopo kwenye maeneo ya Neno la Mungu, zilizoahidiwa katika Biblia, walipewa hiyo nguvu ya kuhuisha, ihuishe hiyo ahadi kwao. Kwa hiyo, waliweka mikono juu ya wagonjwa, wakaponywa. Walinena katika lugha mpya. Walifanya ishara kubwa na maajabu, kwa kuwa hayo yalikuwa katika ahadi ya Mungu. Na wakati Yesu alipokufa, kuwakombolea hayo, ardhi zilizokuwa ni mali ya wana wa Mungu, Yeye alionyesha kile Mungu alichokuwa.

117 Tunathubutuje kulishirikisha hilo kijamii na kuliingiza kwenye madhehebu? Hatuna haki za kufanya jambo hilo.

118 Ni Roho Mtakatifu, leo, akiwinda mioyo miaminifu ambayo itaamini Ujumbe huo. Kila kitu katika Biblia, kilichoahidiwa, ni kwa ajili ya mwaminio huyo. Na wakati unapolikubali hilo katika utimilifu wake, na Mungu anajua ya kwamba utafanya jambo hilo, Yeye anakupa hatimiliki hakiki ya jambo hilo. Ndipo basi kila ahadi iliyoahidiwa ni mali yako, na Roho Mtakatifu yupo hapo apate kuihuisha hiyo kwako. Loo, jamani! Tu—tunapaswa kuwa ni watu wa aina gani? Ni ajabu jinsi gani kuona Roho Mtakatifu mkuu wa Mungu hapa kudhihirisha nguvu hizo! Wazia jambo hilo. Wakati, Roho Mtakatifu Mwenyewe, yupo hapa kuushuhudia wakati huu. Yesu alisema hivyo. Ni yeye yule jana, leo, na hata milele.

Mtu yeyote anathubutuje kufutilia jambo hilo kutoka Humo?

119 "Kazi nizifanyazo mimi ninyi nanyi mtazifanya," Yohana 14:12. "Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio." Hilo ndilo hakikisho. Tunapoliona kundi la watu limeketi pamoja, na ishara hizo zikijidhihirisha zenyewe, hilo ndilo hakikisho ya kwamba ile hatimiliki hakiki iko pale kuthibitisha ya kwamba hao ni mali ya Mungu. Amina.

120 Kwa hiyo, sisi ni Pasaka, pia. Amina. Sasa tuko kwenye Pasaka yetu. Tumefufuka tayari, haleluya, kutoka kwenye mambo ya ulimwengu, mpaka kwenye mambo ya ahadi ya Mungu. Si tutafufuka; tumefufuka. Ni ule uwezekano.

121 Ni ahadi ya Mungu. Yeye atammwaga Roho Wake katika siku za mwisho, na hilo ndilo wangefanya. Angalia, wakaweka mikono yao juu ya wagonjwa; kila kitu kilichokuwa katika ahadi ya Mungu. "Nitaimwaga Roho Yangu katika siku za mwisho, juu ya wote wenye mwili. Wazee wenu wataota ndoto. Vijana wenu wataona maono." Na ahadi zote hizi mbalimbali ambazo alifanya, kila kitu kiko papo hapo katika ahadi ya Mungu. Yesu alitukombolea hizo. Na wakati tunapokuwa . . .

122 Ama, sisi, kama tumekusudiwa mahali hapo, kama tumekusudiwa kuwa mahali hapo; kama yule tai akitembea katika kiota cha kuku. Kama umekusudiwa kuwa mahali hapo,

Roho Mtakatifu yupo hapa kukutafuta. Na wakati anapokupata, unatambua wito Wake. Unajua saa unayoishi. Unajua ya kwamba mambo haya yanapaswa kutukia. Upesi unanyakuliwa upate kukutana Naye, na wewe sasa umeketi katika ulimwengu wa Roho katika Kristo Yesu. Loo, ni ahadi ya jinsi gani! Ni Baba wa Mbinguni wa jinsi gani, Ambaye angetupa mambo haya!

123 Roho anahuisha ushirika wao na Mungu, hivi kwamba wanawafufua wafu, katika siku hiyo. Waliweka miili yao juu ya wafu; wakafufuka. Sikilizeni kwa makini. Walifanya mambo yale yale aliyoyafanya Yesu kwa kuwa Roho yeye yule, aliyekuwa juu Yake, alikuwa juu yao. Kama Roho mmoja akimfanya mtu kutenda hivi, anamfanya huyo mwingine kutenda vivyo hivyo. Kama mmoja . . .

124 Huyu anawezaje kuja juu ya mtu, aseme ana Roho wa Mungu, halafu akane kazi za Mungu? Hawezi kufanya hivyo.

125 Angalia. Uhai wa Mungu, ambao katika Kiyunani unaitwa *Zoe*, ukitenda kupitia kwao na ukiwa ndani yao, ulihuisha nia zao kwa Neno Lake. Sasa, hebu niseme jambo hilo polepole sana sasa. Roho wa Mungu anayetenda kazi miongoni mwa watu, huhuisha nia ya mtu kwenye ahadi ya Mungu. Unaona? Inafanya hivyo. Angalia. Nami ninajaribu kuwaonyesha ile—ile . . . na kuwafanya mtambue ya kwamba ninazungumza sasa juu ya Kanisa, na pia kuhuishwa kwenye Uzima, katika Yeye.

126 Ingawaje, wao walikuwa tu ni sifa Zake, kwanza. Bali kama Mungu alisema, "Katika siku *hii*," nyuma huko mwanzo, "John Doe atakuwa mtumishi Wangu," mamilioni ya miaka iliyopita. Sasa, John Doe amezaliwa katika dhambi, akaumbwa katika uovu, akaja ulimwenguni akisema uongo, kwa maana yeye ni mwanadamu. Lakini, labda, anapata hisia ndogo ya kidini. Ataenda akajiunge na kanisa. Labda atajiunga na kanisa la Kipentekoste. Sijui. Huenda akajiunga na lolote lile. Bali hebu na aingie katika mazingira ya Mungu, wakati mmoja. Unaona? John Doe hana budi kutambua kwamba Baba yake ni Nani, kama tu vile yule tai alivyotambua kwamba mama yake alikuwa ni nani. Hana budi kutambua jambo hilo. Unaona? Ila tu, kwamba John Doe ni sifa ya Mungu ambayo imekuwa neno, lililonenwa, na halafu Roho Mtakatifu analitafuta neno hilo kotekote. Huyu hapa. Anamwita, anampa Uzima wa Milele, na kumwingiza katika Uwepo wa Mungu, Neno la Mungu.

127 Angalia. Mungu alikuwa na jambo lile lile wakati alipomwona Yesu. Ilikuwa ni—ilikuwa ni kazi iliyomalizika ambayo Mungu aliimaliza na Yesu, wakati Yeye aliposema, "Imekwisha." Mpango wote ulimalizika.

128 Na wakati Roho wa Mungu anapokuja juu yako, nawe kwa kweli ni mmoja wa sifa za Mungu alizotamka. Sasa, kama sivyo ulivyo, utatangatanga na kuhangaika, na kukimbia *hapa* na *pale*,

na chochote kile, wala kamwe hutafikia ule ujuzi wa ile Kweli. [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] Kama wewe ni mmoja wa hizo, mambo ya kale yanapita upesi, unaona, nawe unakuwa mpya, na mpango wa wokovu umemalizika. Uko tayari kutii kila Neno ambalo Mungu aliwahi kunena juu yako, unaona, kwamba utatenda. Wewe ni mtiifu kwa Neno Lake. Yale mapatano, hasa, ile hatimiliki hakiki ya mapatano, ile hatimiliki ni mali yako. Deni zote zimelipwa. Zote zimefutiliwa mbali, na kama ilivyokuwa katika Siku ya Pentekoste.

129 Sasa hebu na tuone kule kuhuishwa, hii Roho ya kuhuisha juu ya watu wengine.

130 Sasa, niliwaambia nisingezungumza kwa muda mrefu sana, nami nina dakika ishirini tu kutimiza neno langu, kama nikifanya hivyo, angalieni, kutimiza wakati huo niliosema, kama—kama saa moja.

Angalia basi nguvu hizi za kuhuisha. Ambazo zinakuja tu. . .

131 Sasa, kuna dhihaka nyingi sana za jambo Hilo. Kuna watu wengi sana ambao wanafikiri kweli wanayo, wakati hawana. Watu wengi sana wanafanya jambo hilo kwa sababu wana mawazo ya uongo juu ya yale waliyoona Wakristo wengine wakifanya. Shetani anaweza kuiga yoyote ya hayo. Tunajua jambo hilo. Na kama wamishenari, unaweza kuona hilo likiigizwa: kupaza sauti, kucheza, kunena kwa lugha, mambo haya yote. Unaweza kuyaona yakiigizwa mahali popote. Kweli kabisa. Miongoni mwa makafiri na watu wanaokana kuna kitu kama Yesu Kristo kuwa ni Mwana wa Mungu. Mnaona? Nao wanafanya mambo hayo yote, wenyewe.

132 Lakini Roho halisi na wa kweli anayehuisha anayemjia mwaminio, humhuisha kwenye Neno la Mungu, huko ni kurudi kwenye Chakula cha tai tena, moja kwa moja kurudi mahali anapoishi. "Mtu hataishi kwa mkate tu, bali kwa kila Neno litokalo katika kinywa cha Mungu."

133 Hebu sasa tuone Roho huyu wa kuhuisha wakati anapowajilia watu wengine, kama alivyofanya kwenye—kwenye ile Siku ya Pentekoste.

134 Hebu na tuangalie Pentekoste, jinsi walivyotenda, na tuone kama wao walihuishwa na nguvu hizi za kuhuisha ambazo tunanena habari zake. Kwenye Siku ile ya Pentekoste, wote walikuwa wakingojea kule juu. Kwa nafsi zao, walikuwa wanaogopa. Wayahudi, yale tu watakayofanya, kwa hiyo wakaogopa. Lakini nini kilitokea? Wakati nguvu hizi za kuhuisha ziliposhuka kutoka Mbinguni, kulikuwa na ujasiri uliowakalia. Kulikuwa na jambo fulani, ufahamu fulani, ambapo hawakuwa na hakika sana juu ya jambo hilo saa chache zilizopita. Walijua Yeye alikuwa—alikuwa amekufa.

135 Wanajua alikuwa amefufuka. Walikuwa wamezungumza na Yeye njiani. “Lakini je! jambo hilo liliwahusu wao, ama lilikuwa ni kwa ajili yao tu, kwa ajili ya Yesu Mwenyewe?”

136 Lakini hapa kwenye ile Siku ya Pentekoste, Roho Mtakatifu, yule hatimiliki hakiki alishuka juu ya hao waaminio. Hilo liliwafanya kuwa sehemu ya kufufuka Kwake, likamfanya sehemu ya ushirika Wake. Roho Mtakatifu alikuja na kuwathibitishia ya kwamba watafufuliwa, kwa maana wakati huo walikuwa wamefufuliwa kwa uwezekano, kutoka walio waoga wakawa watu wenye ujasiri.

137 Walikuwa—walikuwa wanaogopa Neno lile lile walilokuwa wamewazia. Msiache hili lipite juu yenu. Walikuwa wakiogopa. Walijua ya kwamba Yeye alikuwa ndiye hilo Neno.

138 Hata Wayahudi ilibidi wakiri jambo hilo. Nikodemo alisema, “Rabi, tunajua ya kwamba Wewe ni Mwalimu aliyetoka kwa Mungu. Hakuna mtu angeweza kufanya mambo ambayo unafanya isipokuwa Mungu yu pamoja Naye. Sasa, tunajua jambo hilo. Tunalitambua.”

139 Kwa hiyo wale wanafunzi. . .Petro alikuwa hata ameapa Mbele Zake. Wote walikuwa wamemwacha pale aliposulibiwa.

140 Bali hawa hapa sasa katika chumba hiki cha juu, katika Uwepo wa Mungu. Ndipo, mara, huyu hapa Roho Mtakatifu anashuka kutoka Mbinguni, Naye akawahuisha. Ndipo kuhuishwa kukatukia, hawakuogopa kuwa mashahidi wa Ujumbe walioamini na kujua kwamba ni wa Kweli. Vinginevyo, waliuogopa.

141 Ni Wapresbiteri wangapi, ni Wamethodisti wangapi, ni Wabaptisti wangapi, walioko ulimwenguni leo, ni Wapentekoste wangapi, wanaoijua ile Kweli na wanaogopa kuchukua msimamo juu Yake? Ninashawishika kushangaa, ni kitu gani hicho kilichowashukia? Je, ninyi ni sehemu ya kufufuka Kwake? Mngethubutu kupaazia sauti nadharia fulani na wazo la mwanadamu? Ama, je! mna ujasiri thabiti na u—uanaume halisi unaohitajika, kusimama na kuita kweli “kweli,” na uongo “uongo”? Je! ninyi ni sehemu ya kufufuka Kwake, ama ni waabudu wa lundo la kanuni za imani? Je! wewe ni mwenda kanisani, je! umejiandikisha jina lako kule, na umekufa katika dhambi na makosa?

Yeye asiyeamini Neno kamili la Mungu ni mwenye dhambi.

142 Wale Mafarisayo waliamini katika mambo mengi, kwamba ni Kweli. Walisema, “Sisi ni watoto wa Mungu.” Nao walikuwa hivyo, mpaka Neno hilo lilipohubiriwa. Lakini wakati Neno hilo lilipohubiriwa na kuthibitishwa, ndipo wakawa wenye dhambi, kwa kukataa Kitu ambacho walijua kilikuwa ni cha kweli, na wakakishuhudia. “Tunajua Wewe ni mwalimu aliyetoka kwa Mungu, kwa maana hakuna mtu angeweza kufanya mambo ambayo unafanya Mungu asipokuwa yu pamoja na Wewe.”

143 Ninashangaa leo, tuko wapi? Nawaulizeni. Ufufuo huu unatukuta wapi? Unathubutu kupiga hatua utoke nje? Unathubutu kumchukua Mungu kwenye Neno Lake? Kama umekusudiwa Uzima, hakika utaliamini. Kama wewe ni tai, huwezi kujizuia kuliamini, kuna Kitu Fulani ndani yako. Ama, je! unataka tu kutumikia kanuni ya imani mahali fulani, useme, "Mimi huenda kanisani. Mimi ni mzuri tu kama ulivyo wewe"? Unaona? Kama huna haki zozote za mzaliwa wa kwanza, kamwe hutaliona, huwezi kuliona. Bali kama unamiliki haki hii ya mzaliwa wa kwanza, huwezi kujizuia kuliona, kwa maana ni sehemu yako nawe ni sehemu yake.

144 Ningewezaje kumkana mama aliyenizaa? Ningewezaje kumkana baba, ambaye damu yake mwenyewe iko ndani yangu? Ningewezaje kumkana Charles Branham kuwa ni baba yangu? Nisingeweza kufanya hivyo. Niko tayari kubeba aibu yake ama chochote kile, kwa sababu mimi ni mwanawe. Haleluya!

145 Basi nikiwa Mwana wa Mungu, Naye alikuwa ni Neno la Mungu, ninawezaje kukana kwamba ile Biblia ni Kweli, kwamba Yesu Kristo si yeye yule jana, leo, na hata milele? Na tukiona saa tunayoishi, tunahitaji Pasaka kanisani. Ufufuo! Tunahitaji ufufuo, kutia imani nguvu, wanaume na wanawake washindanie kile ambacho ni Neno la Mungu lililothibitishwa.

146 Mnasema, "Vema, sisi tunafanya mkutano wetu wa Vijana kwa Kristo." Hilo ni sawa. "Kanisa letu linafanya mkutano. Tunataka wafuasi *kadhaa*." Sina neno dhidi ya jambo hilo. Hilo ni sawa. Bali hayo ni mazingira tu. Hayo yanaweza yakawa ni manyoya ya maskini kuku. Bali kama utaingia katika mazingira yafaayo pale, yatamwangua tai endapo wewe ni yai la tai. Na kama ulichaguliwa tangu zamani na Mungu upate kuliona, huwezi kujizuia kuona jambo hilo, utatokea katika ufufuo. Hivyo ndivyo Mbaptisti alivyozaliwa, hivyo ndivyo Mmethodisti alivyozaliwa, katika ufufuo wa siku hiyo, bali waligeuka wakawa kuku badala ya kuwa tai.

147 Kama nilivyosema si muda mrefu uliopita, nikishuka kutoka Tucson, niliona jambo la ajabu sana. Niliona mwewe ameketi kwenye waya kule. Huyo mwewe amepoteza utambulisho wake zamani sana. Alikuwa ni ndege karibu na tai. Asingeweza kumfuata tai; la, hata kidogo. Hakuna kitu kinachoweza kumfuata tai. Bali alikuwa ni mwewe.

148 Kristo Ndiye Tai, na kanisa linapaswa angalau kuwa mwewe. Wanaweza kuruka juu zaidi kuliko ndege wengine wowote. Lakini huyo mwewe amekuwa mnyonge. Amepoteza utambulisho wake. Yeye huketi kwenye nyaya za simu na kungojea sungura fulani aliyekufa. Anarukaruka kama koho, badala ya kupuruka kama mwewe.

149 Loo, ndugu yangu, dada, enyi Wapentekoste, ambao ni watu wangu wapendwa! Kanisa linapoteza utambulisho wake.

Linashuka na kutegemea kanuni fulani za kawaida zilizokufa za imani, badala ya kupuruka kwenda Mbinguni, huko juu, wapate mana mpya.

150 Huko nyuma mwewe alikuwa akiwinda mana yake mwenyewe, bali siku hizi anaokota kile magari yalichokanyaga na kile koho walacho. Yeye anarukaruka kama koho. Anaonekana kama koho.

151 Sisi tumejipamba sana katika ulimwengu wa kisasa, wanawake wetu wakikata nywele zao, na kuvaa kuptura, wanaume wetu hawana uti wa mgongo wa kutosha kusimama mimbarani na kusema kweli. Tumekuwa wanyonge kwa Neno kitambo sana.

152 Ee Mungu, mtume Roho Mtakatifu na uwatafute hao tai mahali fulani, walio tayari kusimama huko ng'ambo, hata iweje, ambao watapaa waingie anga za anga, si kuketi kwenye nyaya za simu na kutarajia vitabu fulani vya shule ya Jumapili viletwe. Jalia niwe na Neno, na katika upya wa nguvu na dhihirisho la Roho Mtakatifu. Tunahitaji Pasaka, ufufuo ambao ni uwezekano. Rafiki yangu, kama umeridhika na mzoga kama huo wa ulimwengu, kuna kasoro fulani.

153 Dada yangu, ndugu yangu, hebu nikwambie, jambo hili, katika hofu ya Mungu, nikijua ya kwamba huenda nisiishi kuona Pasaka tena. Bali kuna jambo moja la hakika, wakati mwana halisi wa Mungu aliyekusudiwa tangu zamani, kwa Neno la Mungu, anapoisikia Sauti hiyo ya Mungu, yeye atainuka aende akakutane nayo. Ndio uwezekano, ya kwamba ataenda kukutana na Neno halisi lililo hai. Kama Yeye alivyokuwa, Bibi-arusi atamlaki Bwana-arusi. Yeye ni sehemu ya Mwili Wake.

154 Angalia, kitambo kirefu tumeninii, tunapoteza utambulisho wetu. Tunakuja Jumatano usiku, wengine wetu. Wengine wanakaa nyumbani kutazama *Ni Nani Anayempenda Susie*, televisheni, kila namna ya mambo ya kilimwengu, kila namna ya burudani, kukuzuia usiende kanisani. Tumepoteza hilo kitambo kirefu.

155 Seminari zetu, shule zetu, zinatoa kundi la akina Riki wenye theolojia tele, na—na burudani na kila kitu kanisani, kupachukua mahali pa mkutano wa maombi. Tumechukua mavazi na kujaribu kutimiza kile watu wa kisasa wanachojaribu kufanya, kuwaingiza. Kamwe hutawashawishi kwa jambo hilo. Wao wana zaidi ya hayo kuliko uliyo nayo. Hamna shughuli zozote kwenye maeneo yenu...kwenye ardhi yao. Acheni wao waje kwenye yenu, ambako ubatizo wa kweli unaangaza, ambako kuna nguvu halisi za kufufuka. Msijaribu kujenga kanisa kama lao. Msijaribu kuwa na mchungaji kama huyo. Msijaribu kufanya *hili*, *lile*, *lingine*, ama kushirikiana na ulimwengu. Wao wanang'aa kwa Hollywood.

156 Injili ya kweli humeka kwa nguvu. Tai huisikia hiyo. Hawatafuti kung'aa. Wanatafuta mmweko. Kumeka kwa unyenyekevu, kumeka kwa upendo, kumeka kwa nguvu, hayo ndiyo tai halisi anayowinda. Huwezi kukwaruza katika kitalu na umridhishe. Yeye kamwe hataweza kufanya jambo hilo. Kamwe hutamwambia hilo, kwa maana haamini hilo.

157 Hebu hiyo Sauti ingurume kutoka Mbinguni, "Mimi Ndimi niliyekuwa nimekufa, na ni hai tena." Jambo fulani linatukia. "Mimi ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Na itakuwa katika siku za mwisho, nitajimwaga Mwenywe juu ya wote walio na mwili." Utukufu kwa Mungu! "Nitaihuisha lugha yenu ya kibinadamu. Nitazihuisha ndimi zenu za kibinadamu. Nitawapa thibitisho ya kwamba nitawafufua katika ufufuo pamoja na Mimi." Tai wenye mioyo yenye njaa huliendea hilo upesi wawezavyo. Ndiyo Lulu ya thamani kuu, ambayo wanauza vitu vingine vyote, wakainunue. Amina.

158 Mungu na atusaidie, rafiki. Makanisa yetu yanapoteza utambulisho wao.

Hebu na tuendee haraka baadhi yao.

159 Angalia kutenda kwa hao wanafunzi, waliogopa. Walijua Yesu alikuwa ndiye Kweli, lakini, mnaona, ilikuwa ni kinyume cha wazo la wingi wa watu, dini ya wingi wa watu wa wakati huo, dini yenye masharti makali kuliko zote, Masa-. . . Mafarisayo, Masadukayo, na kadhalika, dini zao, makundi, na madhehebu. Walikuwa—walikuwa wanapinga jambo Hilo. "Uzushi." Lakini Yesu alikuwa Ndiye Neno lililotambulishwa.

160 Naye Yesu Ndiye Roho Mtakatifu, katika Roho. "Kitambo kidogo na ulimwengu hautaniona tena. Ninyi mtaniona," sio mwili; Uhai uliokuwa ndani Yake. Mungu yuko juu ya Kanisa, apate kuwaita wana kama alivyofanya wakati huo, watiifu.

161 "Mimi daima hufanya yale yanayompendeza Baba Yangu. Ni nani kati yenu anayeweza kunishtaki kwamba nina Dhambi?" Kwa maneno mengine, *dhambi* ni "kutokuamini." "Neno limesema nini juu Yangu, ambalo sijafanya?" Jambo ndilo hilo. "Nionyesheni yale Neno lilisema kwamba ningefanya, ambayo sikufanya. Ni nani anayeweza kunishtaki Mimi? Ni nani anayeweza kunielekezea vidole vyenu, na kusema ya kwamba sijalitimiza Neno la Baba Yangu?" Loo, wakati kanisa la Kipentekoste litakapofikia kwenye kiwango hicho! "Ni nani anayeweza kunishtakia kutokuamini?"

162 Loo, enyi Wakristo, tambulishweni si kama mwewe, bali tai. Huyo mwewe ni mnyonge, atashuka. Huoni kamwe tai akifanya hivyo. Hatafanya hivyo kamwe. Yeye hujiwindia chakula chake mwenyewe, huko angani. Mungu alimtayarisha kusudi apate kukiona. Yeye hupata mana mpya, si kitu fulani ambacho kimekufa.

163 Katika Waebrania, wakati walipovuka nyika, walikula, walijaribu kula mana iliyoharibika. Ilikuwa imeoza. Ilikuwa na—ilikuwa na vifurukuta mikia ndani yake. Mnajua tunachomaanisha. Imeharibika kabisa, imeoza. Ina mabuu.

164 Kwa nini nile chakula kilichokuwa kimekufa miaka mingi iliyopita? Huenda kikawa katika hali na sura, bali si kipya. Inatupasa kupata chakula kila kizazi, kipya. Vivyo hivyo tai hutafuta chakula hicho, kila kizazi, kwa kuwa tuko safarini mwetu. Angalia.

165 Sasa hebu na tuchukue baadhi ya watu tena. Hebu na tuchukue baadhi ya manabii wa Agano la Kale, tuone kile walichofanya.

166 Hebu kwanza tumwangalie Stefano, jinsi ambavyo Stefano mbele ya hilo Baraza la Wazee. Wakati baraza hilo lilipomleta pale, kusanyiko hilo kubwa la waaminio pale, ama waliodhaniwa kuwa ni waaminio, walipomleta na kujaribu kumhukumu. "Mbona," alisema, "enyi wenye shingo ngumu, wasiotahiriwa moyoni na masikioni, daima mnampinga Roho Mtakatifu." Huo ndio ule Uzima wa Milele. "Kama baba zenu walivyofanya zamani za kale kupitia kwa manabii, ndivyo mnavyofanya siku hizi." Nao wakamsagia meno yao. Hawakutaka kusikia jambo hilo. Yeye alikuwa anapinga kanuni zao za imani. Alikuwa anapinga madhehebu yao. Nao wakampiga mtu huyo kwa mawe akafa. Ndipo akainua mikono yake juu, akaangalia Mbinguni, akasema, "Ninaona mbingu zimefunguka, na Yesu amesimama mkono wa kuume." Kwa nini? Yeye alikuwa na ufufuo, nguvu za kuhuisha ndani yake, zilizomchukua zikampeleka vifuani mwa Yesu.

167 Angalia, upesi sasa. Mwangalie Filipo, kule katika ule ufufuo mkuu. Alikuwa na uamsho mahali ambapo hakuna mtu angalithubutu kuondoka, mbona, kama angalikuwa amepata ushirikiano mkubwa miongoni mwa makanisa na kila kitu kule. Alikuwa na uamsho mkubwa. Na nguvu za kuhuisha za Mungu zikanena naye, zikasema, "Stefano . . . " Labda zilisema hivi, "Wewe una uamsho mkuu, lakini nina mtu mmoja ninayetaka ukazungumze naye."

168 Naye Stefano ni mtiifu, haidhuru ni kitu gani, ukosoaji mwingi kiasi gani. "Loo, Stefano, huwezi kuondoka."

"Lakini, ninaweza. Mungu alisema hivyo."

169 Naye akatoka akaingia jangwani, na huko jangwani akamkuta towashi huyu. Na ni jambo gani lililotukia? Akasema, "Je! . . . Kama unaamini kwa moyo wako wote, ya kwamba Yesu ni Mwana wa Mungu, nitakubatiza." Wakati alipombatiza . . .

170 Angalieni. Yeye alihuishwa na nguvu hizi za kuhuisha, kuacha uamsho wa maelfu ya watu, aingie nyikani, kwa mtu mmoja. Loo, hilo lingekuwa ni kinyume cha hoja zote. Mnaona? "Mbona, kuna watu elfu kumi wanaokutaka uwe *hapa*." Bali

kuna mmoja anayetaka, *huko* nje. Unaona? Na nguvu za kuhuisha zikampeleka hadi mahali palipoandaliwa na Mungu. Haleluya!

171 Enyi wanaume na wanawake, itawafanya msimame kwa miguu yenu. Itawafanya mfanye mambo ambayo Mungu anawataka mfanye. Sijali yale mtu mwingine anayosema juu ya jambo hilo. Jirani anasema, "Loo, mtu huyo amerukwa na akili zake. Wanaomba usiku kucha; wanasoma Biblia." Sijali wanalosema. Ni yale Mungu aliyokuitia kufanya. Hiyo ni kweli. "Loo, wao wanasema hatuwezi kuwa na miamsho hii ya mtindo wa kale wa Kipentekoste." Loo, ndiyo, tunaweza, pia. Unaweza kuwa nao wewe mwenyewe. Na wewe ni walio wengi, katika Mungu, haidhuru hao wengine wanafikiria nini.

172 Angalia, baadaye, katika utiifu. Sikilizeni kwa makini sasa. Baada ya kumtii Mungu, kwa Neno Lake, wakati alipotimiza jukumu lake, nguvu hizo za kuhuisha alizopokea pale Pentekoste zilimnyakua, zikauhuisha mwili wake. Umbali wa maili kadha wa kadha, alitwaliwa katika Roho, naye alionekana katika nchi nyingine mahali fulani. Nguvu za kuhuisha za Mungu! Na kama sisi ni wapentekoste, "Nguvu zile zile zilizomfufua Yesu katika wafu, kama zikikaa ndani ya miili yenu ipatikanayo na mauti." Mnaona? Vema. Angalieni.

173 Hebu na tumchukue mtu mwingine aliye na nguvu hizi za kuhuisha. Kulikuwa na mtu muda mrefu sana uliopita, jina lake Henoko. Wakati jambo jipya lilipozuka, wakati jambo fulani lilipotokea na kusema, "Vema, sasa hatuna budi kurudi kwenye ile shule ya zamani, ama *hili, lile,* ama lile *jingine*," Henoko alitembea na Mungu. Lolote Mungu alilosema lifanywe, Henoko hakukosa hata neno moja. Alitembea na Mungu. Alikuwa ni nani? Alikuwa ni mwana wa Mungu. Alikuwa ni tai aliyeitwa kwenye siku hiyo.

174 Basi wakati ulipowadia, yeye alikuwa amejaa sana nguvu hizo za kuhuisha! Kumbukeni, yeye alikuwa ametembea miaka mia tano, ama zaidi, mbele za Mungu, na hakuna hata wakati mmoja alikuwa amekosea Neno Lake. Hakuna hata wakati mmoja alipotenda mabaya. Hakuna hata wakati mmoja ambapo alitenda lingine ila kudumisha ushuhuda. Kila jambo ambalo Mungu alimwambia kufanya, alienda na akalifanya. Bila kubishana juu ya hilo, alienda tu na kulifanya. Haidhuru mtu mwingine yeyote aliwazia nini, alienda akalifanya. Kwa nini? Alikuwa amejaa nguvu hizo za kuhuisha. Na wakati ulipowadia kwa mzee huyo kufa, Mungu alishusha ngazi tu naye akapanda kwenda Nyumbani. Yeye alimhuisha, kisha akauchukua mwili wake upatikanao na mauti katika unyakuo. Amina. Hizo ndizo zile nguvu za kuhuisha.

175 Mwangalie Eliya, baada ya kazi yake kwisha hapa duniani. Alikuwa amejaa sana nguvu hizo za kuhuisha, alikemea mkato

huo wa nywele mtindo wa Jackie Kennedy katika siku zake. Alikuwa amemwambia maskini Yezebeli mambo aliyowazia juu yake. Aliwaambia hao wahubiri na makuhani yaliyokuwa kweli na uongo, nao hawakumwamini. Bali aliwakemea hao wanawake waliojipaka rangi usoni na kadhalika, kwa ukali. Naye alikuwa amejaa sana hizo nguvu za kuhuisha mpaka hakukuwa na kitu kingaliweza kumdhuru. Mungu alikuwa amemlisha kutoka mbinguni, akamtoa huko na kumtenga kando. Alikuwa amejaa sana nguvu za kuhuisha, wakati wa kufa kwake ulipowadia, Yordani ilifunguka, naye akatembea tu, akatumiwa gari la farasi likamchukua likampeleka Nyumbani, amejaa sana hizo nguvu za kuhuisha. Akawa mwana wa kweli, halisi wa Mungu. Naam.

176 Angalia, yeye alikuwa na mrithi, na jina lake lilikuwa ni Elisha. Naye Elisha alikuwa na sehemu maradufu, nguvu hizi za kuhuisha. Unaona? Alikuwa na sehemu maradufu ya hizo. Sasa, yeye alihubiri kwa karibu miaka themanini, ama alikuwa na umri wa miaka themanini hivi. Alishikwa na ugonjwa na akafa. Sasa, yeye hakupata kwenda Nyumbani kama Eliya alivyoenda. Unaona? Wote wawili wamewakilishwa pale katika Kanisa; baadhi ya watakatifu huondoka, na wengine wanapumzika. Lakini angalia wakati Eliya alipochukuliwa juu katika unyakuo; ndipo Elisha akalala, katika Mungu, amejaa nguvu za kuhuisha. Angalia unabii wake kabla tu hajafa. Unaona?

177 Sasa, hebu niwaonyeshe. Sijali kama umekufa, ama mahali ulipo, nguvu hizo za kuhuisha kamwe haziondoki. Miaka na miaka baada ya kufa kwake, nyama yake ilikuwa imeoza, mabuu ya ngozi yalikuwa yamezila. Lakini walikuwa wamembeba mtu aliyekufa, siku moja, wakamtupa ndani kwenye mifupa hiyo, na kulikuwako na nguvu nyingi sana za kuhuisha mle mpaka mtu huyo akafufuka tena. Haleluya! Zikamfufua katika wafu, kwa sababu nguvu hizo za kuhuisha zilizokuwa juu ya mtakatifu huyo wa Mungu, kamwe hazikumwacha, zilikaa tu juu ya mifupa hiyo.

178 Loo, kumbukeni, sisi ni nyama ya nyama Yake, mfupa wa mifupa Yake, kama sisi ni Bibi-arusi Wake. Kifo hakitatatiza nguvu hizo za kufufuka hata kidogo. "Hata mabuu ya ngozi yakiuharibu mwili huu, hata hivyo katika mwili wangu nitamwona Mungu." Utukufu kwa Mungu! Ni ninii. . . Sijui ninasema nini. Ni tumaini la jinsi gani kwa mtu mzee kama mimi, nikijua ninaona wakati wangu wa mwisho moja kwa moja huko ng'ambo hivi karibuni, nikiwa nina umri wa miaka hamsini na sita.

179 Tangu nilipokuwa mvulana mdogo sana, nimesimama hapa, nikijaribu kutangaza Hili. Lakini ninajua, Kilicho ndani yangu mimi, sina kitu chema, sina kitu nilichofanya. Bali ndani yangu kuna zile nguvu za kuhuisha zilizonihuisha siku moja kutokana na mambo ya ulimwengu, kama kijana, hadi Uzima wa Milele.

Loo, mambo ambayo yametukia! Nimeona maono, nimetabiri mambo. Yeye bado kamwe hajaacha jambo lolote lishindwe. Nimenena kwa lugha zingine. Nimetabiri. Nimefanya mambo hayo kwa Roho wa Mungu aliyekaa ndani yangu. Hizo ni nguvu za kuhuisha. Ninajua ya kwamba siku moja . . .

180 Mkombozi wangu yu hai sasa. Na siku moja wakati atakapokuja, mifupa hii itafufuka tena, iende kukutana na Yeye hewani. Huenda mkanizika baharini, mwiteketeze kwa moto, popote mnapotaka. Nguvu hizo za kuhuisha ni za Milele. Whiu! Ninaisikia Pasaka sasa hivi. Naam, bwana. Nimekuwa nayo kwa miaka. Imo ndani yangu.

181 Iko ndani yenu. Kama, ninyi, Roho aliyemfufua Yesu katika wafu akikaa ndani ya miili yenu ipatikanayo na mauti, amewahuisha kutokana na mambo ya ulimwengu, akawaleta kwenye Neno la Mungu pekee. Amewahuisha kutoka kwenye maisha haya hadi kwenye Uzima wa Milele. Ninyi ambao wakati mmoja mlikuwa mmekufa katika dhambi na makosa sasa mmehuishwa pamoja, kuketi katika ulimwengu wa Roho pamoja na Kristo Yesu, mkila Mana itokayo Juu, mkiuona mkono wa Mungu ukidhihirishwa, kuthibitisha ahadi ya siku hizi.

182 "Kama ilivyokuwa katika siku za Nuhu, ndivyo itakavyokuwa katika kuja Kwake Mwana wa Adamu. Walikuwa wakila, wakinywa, wakioa, wakiolewa. Na kama ilivyokuwa katika siku za Lutu, ndivyo itakavyokuwa katika saa ambazo Mwana wa Adamu atafunuliwa duniani," si Mwana wa Mungu, tena. "Mwana wa Adamu," atakayerudi kama Ujumbe wa kinabii kwa ajili ya siku za mwisho wakati tai huyo atakapokuwa akiruka; si simba; si yule ndama katika ule wakati wa dhabibu. Unaona?

183 Kila wakati, nguvu za kidini zilitoka zikaenda kukabiliana na nguvu za kisiasa za ulimwengu. Wakati simba alipoinuka, zile nguvu za dini, zilienda kukabiliana na nguvu za Kirumi.

184 Na halafu ilipowadia ile saa ya dhabihu, ndama akaenda, kwa maana yeye ndiye Mnyama wa dhabihu wa Bwana.

185 Ndipo wakaja wale watengenezaji, kote kupitia katika nyakati za kanisa, ukaja uso wa mwanadamu. Na watengenezaji walikuwako tangu Luther, Wesley, loo, Calvin, moja kwa moja, kuendelea, wakati wa kipentekoste.

186 Lakini katika Ujumbe wa mwisho uliotolewa, alikuja tai arukaye. Ni wakati wa tai, wakati wa kufunuliwa, Neno la Mungu lililodhihirishwa, Neno la Mungu lililothibitishwa. Loo, enyi watoto, ingieni kwenye ubatizo huu wa Roho Mtakatifu. Ingieni na muuamini Huo, kwa moyo wenu wote, Mungu atawajaza.

187 Angalieni hapa sasa. Tunaona sasa, kumbukeni, "Sisi ni nyama ya nyama Yake, na mfupa wa mfupa Wake." Kama vile Mungu alivyoifufua mifupa Yake na mwili kutoka kaburini,

wao hawawezi kumficha mtu aliye na zile nguvu fiche. Mauti hayawezi kumchukua. Yesu alisema, “Wote alionipa Baba watakuja Kwangu. Nitawafufua katika siku za mwisho.” Loo, jamani! Pasaka! Mbona, tuko moja kwa moja katika Pasaka. Wakati alipofufuka, tulifufuka pamoja Naye. Alituma ile hatimiliki hakiki. Tumeishika, kama ubatizo wa Roho Mtakatifu. “Yu hai milele na milele; yeye yule jana, leo, na hata milele.” Waebrania 13:8 inathibitisha jambo hilo. Ni yeye yule.

188 Watu Wake wa kimasihi, waliotiwa mafuta, wanaamini jambo hilo. Masihi ni nani? Masihi ni nani? *Masihi* ni “Aliyetiwa mafuta.” Na sasa kama Yeye alikuwa ni Masihi, kwa kuwa Aliyetiwa mafuta kwa siku hiyo, kulitimiza Neno la Mungu, apate kuwa Mkombozi na Aliyetiwa mafuta, na Mungu akaufufua mwili huo; Bibi-arusi Wake ndiye mtiwa mafuta kwa ajili ya siku hii. Tayari amefufuliwa pamoja Naye katika ule ufufuo, kwa sababu, “Hawa wawili ni mmoja.” Amina.

189 La—laiti ningaliweza kulieleza jinsi ninavyoliona. Laiti ningalikuwa na elimu ya kulielezea. Unaona? Na—natumaini mnaliona. Natumaini, Mungu, Roho Mtakatifu anashuka hapo na anaweka hilo moyoni mwako, upate kuona ninalomaanisha.

190 Ufufuo, sasa hivi tuko katika ufufuo. Tumeketi pamoja na Yeye katika ufufuo, bali ni wale tu walio na Uzima.

191 Si wale wasio na Uzima. Hawatajua jambo Hilo. Hawatalijua kamwe. Wataendelea moja kwa moja wakifikiri ya kwamba wanampokea Roho Mtakatifu, wanaokolewa, nao Unyakuo utakuwa umetukia na umekwisha. Kasema, “Eliya amekuja tayari, nao wakafanya hivyo, wala hamkujua.” Unaona?

192 Angalia. Mauti haizikomeshi nguvu za Mungu za kuhuisha. Angalia. Mauti haiwezi kuzikomesha.

193 Unasema, “Vema, mama yangu alikuwa ni mwanamke aliyejazwa Roho. Baba yangu, sijapata kuona mtu aliyejazwa na nguvu hivyo kama baba yangu. Lakini alikufa, Ndugu Branham.” Hakika. Hilo halikuzikomesha nguvu hizo za kuhuisha.

194 Musa alikuwa na nguvu hizo za kuhuisha. Mnaamini jambo hilo? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Hapajapata kuwapo na mtu kama yeye duniani, mpaka Yesu. Kwa kuwa hakuona tu maono, alizungumza uso kwa uso na Mungu.

195 Hata nabii mke, Miriamu, alishindana na neno lake siku moja. Yeye akasema, “Hivi humwogopi Mungu? Mtafakarini mtumishi wangu, Musa. Hakuna mtu ulimwenguni kama yeye, wakati huu. Hapajatokea mtu kama Musa. Mimi ninasema na Musa. Je! yeye alisema nini, ambalo halikuwa ni kweli? Mnaona? Ninanena na Musa. Hivi humwogopi Mungu? Kamwe usiseme neno dhidi yake.” Na papo hapo akapigwa na ukoma na—na alikuwa yuafa. Hakuishi muda mrefu sana, baadaye. Musa alimwombea.

196 Ndipo Musa akakwea mlimani, akiwa na miaka mia moja na ishirini ya huduma, ama miaka themanini ya huduma; miaka mia moja na ishirini ya maisha, akapanda mlimani na akafa, na akazikwa bondeni. Lakini nguvu hizo za kuhuisha zilikuwa juu yake. Kama miaka mia nane baadaye, huyu hapa, amesimama juu ya Mlima wa Kugeuka Sura. Amina. Alikuwa ni nani? Yeye alihesabiwa katika ule ufufuo. Hakika, alihesabiwa. Alikuwa na nguvu za kuhuisha za Mungu. Huyu hapa, amesimama.

197 Waangalie Ayubu, Ibrahimu, Isaka, wale watakatifu katika ile siku ya kufufuka, ile asubuhi kuu ambayo Ayubu na hao wote walijua ya kwamba itakuja. Wakati, yeye aliposema, "Ninajua Mkombozi wangu yu hai," mamia na mamia ya miaka kabla ya Kristo. Ni ninii, kwa kweli, Kitabu cha Ayubu kiliandikwa kabla ya kile cha Mwanzo, ndivyo wanavyodai, ndicho Kitabu cha kale kabisa katika Biblia.

198 Na katika majaribu yake, na kama yale tunayopitia sasa. Na mke wake, hata, kitu kilichokuwa karibu sana naye duniani, alisema, "Mbona usimkufuru Mungu ukafe mauti?"

199 Akasema, "Wewe wanena kama mwanamke mpumbavu. Bwana alitoa, Bwana ametwaa, Jina la Bwana libarikiwe."

200 Na ndipo wakati Roho wa Mungu alipokuja juu yake, na akaanza kutoa unabii, alisema, "Ninajua Mkombozi wangu yu hai, na katika siku za mwisho atasimama juu ya nchi hii. Hata mabuu ya ngozi yakiuharibu mwili huu, hata hivyo katika mwili wangu nitamwona Mungu." Ndipo akajitengenezea mahali pa kujizika. Akasema, "Tutanunua shamba hili." Akalinunua hapo na akajizika mwenyewe.

201 Baadaye, akaja mtu jina lake Ibrahimu. Kanisa linakua, linaongezeka. Ibrahimu, vema, sasa, alikuwa na nguvu fiche za Mungu, pia, Uzima wa milele, wa Milele, kwa maana Mungu alimwita. Sasa angalia. Wakati alipokufa, ama Sara alipokufa, alinunua kipande cha shamba huko Palestina, karibu na kaburi la Ayubu, na akamzika Sara. Ibrahimu akafa naye pia akazikwa pamoja na Sara. Ibrahimu alimzaa—alimzaa Isaka.

202 Na Isaka, wakati alipokufa, alilala pamoja na Ibrahimu, katika kipande kile kile cha ardhi. Sasa, wakati, Isaka akamzaa Yakobo.

203 Yakobo akafa, huko mbali Misri. Lakini kwa kuwa alikuwa ni nabii, sasa, akiwa na nguvu hizi fiche, nguvu hizi za kuhuisha, alisema, "Usije ukanizika huku, Yusufu. Njoo hapa, mwanangu nabii. Weka mkono wako kwenye nyonga hii ambayo Mungu aliilemaza. Apa kwa Mungu wa Mbinguni hutanizika huku." Ni kitu gani kilichokuwa ndani ya mtu huyo? Kwa nini Misri haikuwa inafaa tu kama mahali pengine popote? Yeye alikuwa ni nabii. Alijua mahali ambapo ufufuo huo utakuwa. Haukuwa unaenda kufanyika huko Misri; utakuwa huko Palestina. Akasema, "Weka mikono yako kwenye nyonga yangu

iliyolemazwa, na uniapie kwa Mungu ambaye nimemtumikia. Wewe ni mwanangu nabii, ya kwamba, hutaizika mifupa yangu huku. Utanipandisha unipeleke kule ukanizike."

204 Yusufu, akiwa nabii, pia, aliweka mikono yake juu ya baba yake aliyelemaa. Akasema, "Ninaapa kwa Mungu wa Ibrahimu, Isaka, wa Yakobo, sitakuzika hapa." Wakamchukua na kumzika katika nchi hiyo. Kwa nini? Kwa nini?

205 Wakati Yusufu alipokufa, alisema, "Msinizike hapa. Msinizike hapa." Kwa nini? Mungu ni Mungu kila mahali, lakini Yeye ana mpango fulani. Yusufu alikuwa ni nabii. Akasema, "Siku moja," sikilizeni, maneno yake, "Bwana Mungu tena atawazu-. . .atawazuru, naye atawatoa kwenye nchi hii. Na mtakapoondoka, mwichukue mifupa yangu."

206 Hizo nguvu za kuhuisha zilikuwa kwenye mifupa hiyo. Loo! "Kama Roho Wake Yeye aliyemfufua Kristo katika wafu, akikaa ndani yenu, Yeye pia ataihuisha miili yenu ipatikanayo na mauti."

207 "Msiiweke mifupa yangu huku. Izikeni kule pamoja na hao wa ahadi."

208 Yesu alipokuja, hapa, nina Andiko hapa, Mathayo 27:51. Wakati Yesu alipofufuka katika wafu, Ayubu aliona hilo likija, akasema, "Ninajua Mkombozi wangu yu hai. Siku za mwisho, Yeye atasimama juu ya nchi hii. Ingawa mabuu ya ngozi yameuharibu mwili huu, hata hivyo katika mwili wangu nitamwona Mungu. Nitamwona." Wao walijua. Huyo alikuwa ni nabii. Ibrahimu alikuwa ni nabii. Isaka alikuwa ni nabii. Yakobo alikuwa ni nabii. Yusufu alikuwa ni nabii. Nao walikuwa na ufunuo wa Mungu, kulingana na Neno Lake. Na kwenye asubuhi hiyo ya Pasaka, wakati Huyo alipokuja na kuwakomboa wale wote waliokuwa wamemwamini, walifufuka, pia, kulingana na Biblia.

209 Nguvu hizo za kuhuisha ziliingia katika kaburi la Ayubu, ambamo hata hamkuwa na kijiko kimoja cha mavumbi ya mifupa yake yaliyobakia. Baada ya hayo mamia na mamia na mamia ya miaka, mifupa yake ilikuwa imeoza. I—ilirudi, na kugeuka kuwa gesi za duniani, na ni vumbi tu la majivu lililokuwa pale. Lakini, hata hivyo, wakati hizo nguvu za kuhuisha, kulingana na Neno la Mungu, kwa ile ahadi, mamia na mamia, naam, maelfu ya miaka baadaye, wakati nguvu hizo za kuhuisha zilipoletwa kutoka kaburini; Ayubu, Ibrahimu, Isaka, Yakobo, wote hao, walitoka kaburini pamoja Naye.

210 Biblia ilisema hivyo. Mathayo Mtakatifu, mlango wa 27 na kifungu cha 51, ilisema, "Watakatifu wengi waliolala katika mavumbi ya ardhi, walifufuka na wakatoka makaburini pamoja Naye, wakati alipofufuka kwenye asubuhi ya Pasaka." Kwa nini? Walikuwa na hizo nguvu fiche. Walikuwa na hizo nguvu za kuhuisha, unaona, nao wakafufuka katika wafu, nao

wakaambatana pamoja Naye katika ule ufufuo. Wakaufurahia ufufuo huo pamoja Naye, kwa kuwa walikuwa wamejaa nguvu hizo za kuhuisha. Walikuwa na ule muhuri halisi wa Pasaka.

"Vema," unasema, "laiti ningaliishi huko nyuma katika Agano la Kale."

211 Ngoja kidogo. Katika Wathesal-. . . wa Kwanza, Wathesalonike, mlango wa 4, kifungu cha 16, ninataka msome hicho. "Sitaki msijue habari zao, ndugu, waliolala mauti, msije mkahuzunika, kama na wengine wasio na matumaini. Maana ikiwa twaamini ya kwamba Yesu alikufa, na akafufuka tena siku ya tatu," si kujifanya waaminio, bali tunaamini hilo, "vivyo hivyo na hao walalao katika Yeye Mungu atawaleta pamoja Naye."

212 Watakatifu wa Agano Jipya walio na nguvu hizo za kuhuisha, watafufuka, pia, katika Kuja Kwake mara ya pili; hakika tu kama vile wale watakatifu wa Agano la Kale wakiwa na nguvu zote hizo za kuhuisha kwenye mifupa yao, na kubadilishwa na zile nguvu, na kadhalika, zilizoonyeshwa na Mungu. Hao manabii ambao walijiliwa na Neno la Mungu, walifufuka pamoja Naye kwenye asubuhi ile ya ufufuo; na pamoja na ahadi ya Mungu ya kwamba kila mmoja aliye katika Kristo Yesu atakuja pia pamoja Naye katika kufufuka Kwake, zile nguvu za kuhuisha za Mungu zikiwa kwenye mifupa hiyo.

213 Si ajabu, tunaweka mikono juu ya wagonjwa. Si ajabu, tunapendana. Sisi ni ndugu na dada. Haitupasi kuchukiana kwa sababu tunasahihishwa na Neno la Mungu. Inatupasa kupendana, na kuheshimiana mmoja kwa mwingine. Unajua, usipofanya hivyo, halitakusaidia.

214 Kuna jamaa mdogo anayeketi papa hapa, ambaye, yuko kwenye kanisa hili sasa. Siku chache zilizopita. . . Mtu huyo anaamini. Maskini mvulana huyo mdogo alikuwa na kansa sikioni mwake, wala asingesema jambo lolote kuihusu. Alikuwa akifanya kazi pale nyumbani. Nilikuwa kwenye ziara ya kuwinda pamoja naye, huko kwa ndugu wa Moseley, na Ndugu Dawson aliyepo hapa. Tulikuwa juu huku tukiwinda, mwana wa Ndugu William. Ndipo ilitokea kwamba niliangalia sikio lake, na nikaona sikio lake lote limevimba. Nikasema, "Kuna nini, Donavan, sikio hilo?"

215 Akasema, "Ndugu Branham, limekuwa hivyo kwa muda mrefu. Sijui."

216 Ni—nilimshika tu mkono pale. Hiyo ilikuwa ni kansa kubwa sikioni mwake. Sikusema neno hata moja; niliushika tu, na kuwazia, "Ndugu yangu!" Katika muda wa siku moja ama mbili baadaye, hapakuwa hata na kovu la hiyo lililosalia. Ilikuwa ni heshima yake kwa Mungu wa Mbinguni, kwa nguvu Zake za kuhuisha, ziliua kansa hiyo na kuyahifadhi maisha ya Donavan Weerts hapo nyuma. Hiyo ni kweli.

217 Mambo haya ni nini? Angalieni hapa, watu walioko hapa Phoenix. Angalieni ninyi watu ambao mmeamini hili. Angalieni watu walio na hili, wanaowawekea mikono yao. Angalieni kinachotukia. Ni nguvu za kuhuisha. "Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio." Wakiweka mikono yao juu ya wagonjwa, nguvu hizo za kuhuisha, tai kwa tai, jambo fulani litatukia. Sasa, tai kwa koho, haitafaa kitu. Tai kwa tai, wanainuka kutoka kwenye kitalu, kuingia Anga za juu. "Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio," wakati wote wameamini.

218 Angalieni nguvu zizo hizo za kuhuisha za Mungu zilizowakilishwa katika manabii hawa wawili, Eliya na Elisha. Angalia, neno lile lile; mmoja wao anatwaliwa juu, huyo mwingine ananyakuliwa. Kunyakuliwa na kutwaliwa. Mnaona? Yeye alitwaliwa. Sisi tutanyakuliwa; tutanyakuliwa pamoja nao, kuwalaki hewani. "Tutanyakuliwa kuwalaki hewani."

219 Angalia, ndege hana budi kuwa na mabawa mawili, kujiweka usawa. Hiyo ni kweli? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Eliya alikuwa ndiye bawa la kuhamishwa, Eliya. Elisha alikuwa bawa la ufufuo. Unaona? Wote wawili, pamoja, wakiwakilisha watakatifu walio hai na watakatifu ambao wameaga dunia.

220 Kumbukeni, walihuishwa kuona yaliyopita, yale mapazia. Jinsi watu hawa walivyohuishwa huko nyuma wapate kuangalia ng'ambo ya pazia na kuona kotekote mpaka wakati huu; hao manabii!

221 Mwangalieni Paulo, alisema katika siku za mwisho jinsi ambavyo watu hawa wangekuwa, wangetenda na kujiita wenyewe Wakristo. Yeye alikuwa ni nabii, aliyejaa nguvu za kuhuisha, alitangulia kuona hilo likitimia. Tunaamini hilo. Sivyo? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Yeye alipokea nguvu za kuhuisha.

222 Angalieni hizo nguvu za kuhuisha leo, zikitabiri mambo, pasipo kukosea tukio hata moja. Hakuna hata wakati mmoja linapokosea. Nguvu za kuhuisha; si nguvu za mwanadamu; nguvu za Mungu. Zile nguvu, ile hatimiliki hakiki ya Pasaka, Yesu aliyefufuka ambaye alituma tena ile hatimiliki hakiki, kutuhakikishia ya kwamba tayari tumehuishwa pamoja Naye.

223 Angalia. Mnakumbuka kile kitabu kidogo, Wafanyabiashara hapa, *Kuangalia Nyuma ya Pazia la Wakati*? Ninaanza kuzeeka, nikijua siku zangu zinapungua. Ninakuwa ninii sana . . .

224 Ninafungulia huo wimbo ambao hao mabibi waliimba kitambo kidogo kilichopita. Nimekuwa nao kwa karibu miaka kumi na nane, ishirini sasa. *Napenda Kulizungumza Kwa Undani, Bwana*. Na kutoka hapo kuingia kwenye maombi, ndipo hizo nguvu za kuhuisha zinakuja. Ninapumzika. Nikaangalia Kule juu. Nasema, "Angalieni kule juu."

225 Ninakumbuka asubuhi ile, nilipotwaliwa ng'ambo. Na mke wangu, ameketi kule nyuma, akiwa amelala kwenye kitanda kimoja pamoja na mimi asubuhi hiyo. Niliamshwa, na nikaangalia juu. Na huyo hapo, amelala. Nikasema, "Kama nitamfanyia Bwana jambo lolote, itakubidi kuharakisha, kijana. Umepita umri wa miaka hamsini." Ndipo Roho Mtakatifu akanitwaa, nami nikaangalia huko Ng'ambo ya pili. Nikawaona hao watakatifu, hakika tu kama ninavyosimama hapa karibu na dawati hili, na Kitabu hiki kitakatifu kikiwa hapa, na mhudumu wa Injili.

226 Je! nimepata kuwaambia jambo lolote katika Jina la Bwana ila lile lililotukia? Kama niliwaambia, ninataka mniambie juu yake. Kila wakati, je! limekuwa ni kamilifu, jukwaani? Kila wakati, je! limetukia kama tu vile alivyosema? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Hii ilikuwa ni BWANA ASEMA HIVI.

227 Nilisimama pale, nikaangalia ng'ambo wakati huo. Nikaona makumi elfu mara maelfu wakija, vijana wanaume na wanawake, wakikimbia, wakinikumbatia, wakipaza sauti. Nikaangalia moja kwa moja nyuma na kujiona mwenyewe nimelala kitandani. "Ee Bwana, nijalie niangalie nyuma ya pazia la wakati."

228 Ni kitu gani? Ni nguvu za kuhuisha zitakazotunyakua. Hizo nguvu kuu za kuhuisha. Nguvu za kuhuisha zimekuja katika siku hizi za mwisho.

229 Hilo ndilo kusudi langu la kuwa hapa Arizona, sasa hivi. Kuna watu wengi walioketi papa hapa, waliosimama papa hapa Phoenix, na kunisikia nikiwaambia kutoka kwenye jukwaa lili hili, "BWANA ASEMA HIVI." Ni wangapi wanakumbuka hilo? "Sasa nenda. Jambo fulani liko karibu kutukia."

230 Niliona Malaika saba wakija. Hivi si gazeti la *Life* lililiandika, wakati ukungu Wake ukielea kupitia huku, umbali wa maili ishirini na saba kwenda juu, na maili thelathini mlalo? Hivi Fred Sothmann, hawa wengine, Gene Norman, hao, si wanaketi huko nyuma? Walisimama papo hapo wakati hao Malaika saba walipotokea papo hapo kilimani. Lilitikisa vilima, kwa maili kadhaa mahali pale, namna hiyo. Malaika saba walisimama hapo. Na kukutupia upanga mkononi mwako, kasema, "Nenda nyumbani na ukafungue hii Mihuri Saba ambayo imetolewa." Nayo hii hapa, siri ya kweli juu ya ndoa na talaka, na uzao wa nyoka, na mambo haya yote ambayo yamebishaniwa. Ni BWANA ASEMA HIVI.

231 Ni kitu gani? Nguvu za kuhuisha zikija Kanisani, zikilitayarisha, saa hii tunayoikaribia. Nguvu za kuhuisha!

Ee Mungu, tusaidie kuzipokea. Tusaidie kuziamini.

232 Unaona, inategemea unalichukua kwa msimamo gani, kama zitakusaidia kwa chochote, ama hazitakusaidia, hata

hivyo. Unaona? Huna budi kuamini jambo Hilo. Usipoliamini, halitakufaa hata kidogo.

233 Jinsi ambavyo maskini Samweli alivyosimama pale mbele ya watu hao, na kusema, “Je! nimepata kuwaambia jambo lolote katika Jina la Bwana ila lile lililotukia? Je! nilipata kuwaomba pesa zenu, kwa matumizi yangu?”

“La, bali tunataka mfalme, hata hivyo.”

234 Hivyo ndivyo kanisa lilivyo siku hizi. Wanataka mawazo yao wenyewe. Hawatakusikiliza hata kidogo. Wanaondoka tu. Vema, inaonyesha tu, zile nguvu za kuhuisha haziko.

235 “Loo,” unasema, “Vema, nilinena kwa lugha. Niliruka na kupaza sauti.” Hayo yote ni mazuri.

236 Bali kama nguvu hizo za kuhuisha ziko, utatambua. Kama yule tai mdogo; huyo ni mama yake. Hilo ni Neno. Hilo ni BWANA ASEMA HIVI. Hilo ndilo Mungu aliloahidi. Hilo ndilo lililotabiriwa. Hilo ndilo lililotukia hasa. Hatuna shaka kabisa, kwa uwezekano tuko katika ufufuo sasa hivi, watakatifu wakijiweka tayari kunyakuliwa hewani.

237 Kwa hiyo, Yesu, akiwa amejaa sana nguvu hizi za kuhuishwa, alisema, “Kama mnaweza kuliharibu hekalu hili; ambalo liliwachukua miaka arobaini, mliyofikiria, kulijenga; nitalisimamisha katika siku tatu.”

238 Kwa nini? Ni kwa nini Yesu angeweza kusema jambo hilo? Nataka kuwauliza. Ni kwa nini Yesu angeweza kusema jambo kama hilo? Yeye alijua ya kwamba alikuwa Ndiye. Amina. Laiti ningeliweza kufanya jambo hilo lishikilie. Yeye alijua kwamba alikuwa ni Nani. Alijua jambo hilo, kila Neno, Mungu alilokuwa ameandika humo ndani juu Yake, Yeye alikuwa amelitimiza. Alijua Yeye alikuwa ndiye Yule Daudi aliyenena habari Zake.

239 Je! mnajua ninyi ndinyi Biblia inayonena habari zenu? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Je! unajua nafasi yako iko katika Kristo? Kama wewe uko katika Kristo, wewe ni kiumbe kipya. Je! unajua Neno hili ni kama tu maisha ya kila siku, kwako? Mbona, hakika. Ni lako. Wewe ni tai. Hilo ndilo Chakula chako.

240 Alijua kwamba, kwa nguvu za Mungu, Yeye angefanya hivyo, kwa sababu ilitabiriwa ya kwamba Yeye angefanya hivyo. Hiyo ndiyo sababu yeye hakuogopa kusema, “Liharibuni hekalu hili. Nitaliinua katika siku tatu, kwa maana Daudi alisema, ‘Sitaiacha nafsi yake katika kuzimu, wala sitamwacha Mtakatifu Wangu aone uharibifu.’” Alijua hakuna seli hata moja ya mwili Wake ingeharibika. Nayo huharibika katika saa sabini na mbili. Alisema, “Liharibuni hekalu hili. Nitaliinua tena, katika hizo siku tatu.” Kwa nini? Alikuwa amejaa sana nguvu hizo za kuhuisha zilizohuisha kila Neno. Aliangalia nyuma na

akaona kila Neno Mungu aliloandika kumhusu Yeye, na nabii alisema Yeye alilitimiza. Alijua hilo lingetimizwa, pia.

241 Sasa, kila Neno ambalo Mungu alisema, je! roho yako imesema "amina" kwake, limetimizwa katika maisha yako, kama mwaminio?

242 Je! unashikilia jambo fulani, unasema, "Vema, kanisa langu linafundisha tofauti"? Basi kuwa mwangalifu, ewe mwewe.

243 Angalia. Tai wanaamini. Hakuna swali, kwao. Wanaliamini. Angalia.

244 Sasa, Yeye alijua lingetukia kwa sababu Neno lilisema lilikuwa litukie hivyo. Na kila Neno lililoandikwa juu Yake ilibidi litimizwe. Alijua ya kwamba liliandikwa kwa uwezo wa Mungu, na manabii watakatifu waliokuwa wametabiri ya kwamba Yeye angefanya hivyo.

245 Na unabii kamwe haushindwi. Hauwezi kushindwa. Neno la Mungu haliwezi kushindwa. Nalo limeandikwa katika. . . na Roho ya kwamba. . .Na sasa, pia, Roho aliyemfufua Yesu katika wafu, kama akikaa ndani ya utu wako, mwili wako, pia atauhuisha mwili wako upatikanao na mauti. Basi, hebu upige risasi, uchome moto, ufanyie lolote utakalo, uudhihaki, urarue, ukatae, ufanyie unachotaka kuufanyia. Mungu ataufufua, kwa kuwa alisema ataufufua. Na kila mtakatifu wa Mungu aliye na ahadi hiyo ndani yake, anajua ya kwamba hilo ni Kweli. Kwa hiyo, usiogope, ndugu, tayari tuko katika Pasaka.

246 Angalia sasa kwenye kule kugeuka Sura, kabla tu hatujafunga. Geuza sura, kugeuka sura, sisi sote tumewakilishwa pale kwenye kugeuka sura. Hebu angalia kile tunachoona siku hizi. Angalia tu kile tunachoona siku hizi, zile nguvu za kuhuisha za Mungu. Sote tulikuwa pale. Kulikuwako na wale watakatifu waliokufa, wamewakilishwa katika Musa; kulikuwako na ufufuo; na Yesu Kristo aliyetukuzwa. Elisha. . . Musa, Eliya, na Yesu, wote wamesimama mlimani; watakatifu waliokufa, watakatifu walionyakuliwa; na Yesu aliyetukuzwa. Loo, jamani!

247 Vema, unasema. . .Nilimsikia jamaa fulani akisema. Watu watasema, "Enyi watu, mbona, kama mlikuwa na nguvu za namna hii, mnapaswa kutoka kwenda na kuwaambia watu yale mnayoweza kufanya." Na iwe mbali na Mkristo halisi, kusema kitu kama hicho. Unaona? Hakika, hatudai nguvu zozote. Kuninii. . .

248 Bali tunafanya jambo moja. Wakati wao walipoangalia pande zote, wakiwa na nguvu hizi zote juu yao, "Walimwona Yesu peke yake." Na mwaminio halisi, wa kweli hajali kama anayatetea madhehebu, ama hahusiki kwa chochote. Yeye anataka tu jambo moja, wewe umwone huyo Kristo aliyetukuzwa, inafanya tofauti yoyote. Tukio halisi, la kweli la Mlima wa Kugeuka Sura humtukuza Yesu Kristo tu.

Halikumtukuza Musa, halikumtukuza Eliya, hawakujitukuza wao wenyewe, halikutukuza chochote kile, bali walimwona Kristo aliyetukuzwa. Na mwaminio yeyote wa kweli, hilo ndilo lililo katika moyo wake, kumtukuza Yesu Kristo. Hilo ndilo analojaribu kuwafanya watu waone.

249 Si kusema, "Vema, kama ukija ukajiunga na makundi yetu, kama ukija na kufanya *hili* ama kufanya *lile*." Loo, usifanye jambo hilo. Usifanye jambo hilo.

250 Angalia Neno la Mungu, ambalo ni Kristo, aliyetukuzwa; na kutimiza ahadi ya siku hii, katika saa hii kuu ya ufufuo. Angalia. Na linawapa furaha, kujua ya kwamba sisi tuko pamoja na Yeye, nyama ya nyama Yake, na mfupa wa mifupa Yake. Ni furaha ya jinsi gani! Hilo ndilo jambo pekee ambalo mwaminio wa kweli hujali kuhusu.

251 Hawajali juu ya madhehebu. Hawajali kuhusu shirika. Hawajali juu ya yale wanawake wengine wanafikiri. Hawajali. Hakika hawajali. Hawatafanya mambo haya ambayo ninii... wanawake hawa wengine wanayofanya. Wao...Wanaume hawa hawatafanya mambo hayo. Hawatakaa na kuchezacheza na madhehebu fulani, wajihadhari wasije wakafukuzwa, na kuogopa hawatapata tikiti ya posho. Hawajali juu ya mambo hayo. Ni upuuzi kwao.

252 Kuna shauku moja tu ya moyo, hiyo ni, kumwona Yesu Kristo akitukuzwa. Matendo yao hayana budi kuambatana na Mungu. Inabidi kabisa yawe, si kitu kingine, bali ni utukufu wa Yesu Kristo pekee. Na Yesu ni kitu gani? Ni Neno. Hiyo ni kweli? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Sasa, angalia, na tukiona njia yake ile ile iliyothibitishwa, akithibitisha ufufuo Wake. Sasa ni kitu gani? Kuona maisha yako, kwa Neno Lake lililoahidiwa ambapo Yeye alisema, "Ni yeye yule jana, leo, na hata milele," akithibitisha ya kwamba Yeye angali hai.

253 Sijali kama kila mlango nchini umefungwa kwangu. Hiyo, mimi ni...Kama nilivyosema, nilikuwa na umri wa miaka hamsini na sita, hivi majuzi. Ningeweza kuondolewa ghafla. Niko kwenye umri wa kushikwa na ugonjwa mbaya wa moyo. Niko kwenye umri huu wote mwingine, na chochote kile. Vema, kuna tofauti gani? Halikuleta tofauti yoyote kwangu nilipokuwa mtoto mdogo. Halileti tofauti yoyote sasa, kwamba namba yangu itaitwa wakati gani, na kadi yangu kutolewa kwenye rafu. Sijali kama watu walipata kujua kama nilipata kuishi duniani. Kwangu haileti tofauti hata kidogo. Si muhimu wawe na minara mikubwa ya ukumbusho na majengo makubwa kutangaza ya kwamba niliishi hapa duniani.

254 Jambo moja tu ninalowataka wajue, kujua ya kwamba "Yesu Kristo ni yeye yule jana, leo, na hata milele." Na katika moyo wangu ninashikilia hatimiliki hakiki Yake. Nami ninajua ya kwamba siku moja...Ingawa, huenda nikafa maji

baharini. Huenda nikauawa huko Afrika. Sijui litakalonipata. Bali ninajua jambo moja, nina ile hatimiliki hakiki. Haleluya! Kila mlango unaweza kufungwa. Hilo halileti tofauti yoyote kwangu. Sijaribu kumtukuza mtu fulani au madhehebu fulani, wala mimi mwenyewe, ama kundi lolote, ama chochote kile. Ninataka watu wamwone Yesu Kristo amefufuka katika wafu, na Roho Wake anaishi, "Ni yeye yule jana, leo, na hata milele."

255 Si ajabu, Yesu alisema, "Usiogope. Mimi Ndimi niliyekuwa nimekufa, bali ni hai hata milele na milele."

256 "Kwa kuwa sasa tumekombolewa Naye, na tumefufuka pamoja Naye, na sasa (si tutakuwa) tumeketi katika ulimwengu wa Roho katika Yeye." Sasa, tunapokuwa na Roho huyu ndani yetu, ile hatimiliki hakiki, inaonyesha ya kwamba tashwishi zote zimeondolewa. Ni kitu gani? Kristo anaishi. Si kwamba *mimi* ninaishi; si *mimi*. "Kristo anaishi ndani yangu." Si *wewe* unayeishi, bali Kristo anaishi ndani yako; kwa sababu Neno Lake lililo hai linaishi ndani yako, likionyesha ya kwamba hesabu yote ya mawazo yako ya Kimethodisti, na ya Kibaptisti, na ya Kipentekoste, chochote kile, vilifutiliwa mbali. Na Yesu Kristo . . .

257 Kama vile kwenye Mlima wa Kugeuka Sura, manabii wote na mengine yote yamekoma. Siku zote za Kilutheri, Kimethodisti, Kipresbiteri, zote ni sawa, lakini, "Huyu ni Mwanangu mpendwa. Msikieni Yeye," Neno la wakati huu, wakati wa ile Mihuri. Wakati, siri zote za kule nyuma, ambazo zimefichwa miaka hii yote, hizo ni piramidi ile kuu ya wakati iliyoondolewa, jiwe la kifuniko, kuifanya hiyo ichongoke kusudi ile nyota ya Daudi ikae mahali Pake. Na lile Kanisa kuu la Mungu aliye hai litainuliwa kama mbawa za tai, lichukuliwe lipelekwe Utukufuni. Naam.

258 Ndani sasa, ndani sasa, ndani ya miili yetu: pamoja na kunena kwa lugha mpya; pamoja na kutabiri, na kuona ya mbele; kuweka mikono juu ya wagonjwa, nao wanapona; ulimwengu, umekufa, na mambo yote ya ulimwengu. Tumepita toka mautini kuingia Uzimani, na sasa tunashikilia zile nguvu. Haleluya!

> Kwenye asubuhi hiyo ya ufufuo,
> Wakati mihuri ya mauti itakapovunjwa,
> Tutafufuka, (Haleluya!) tutafufuka. (Amina!)

259 Hakuna pepo wa kutosha kuzimu kutuzuia tusifufuke. Tulichaguliwa tangu zamani na Mungu kwa wakati huu. Neno la Mungu linajidhihirisha Lenyewe moja kwa moja kupitia kwetu. Nasi tunaishi katika Uwepo wa Mungu, kwa ahadi ya Neno la Mungu. Hakuna pepo kuzimu anayeweza kunizuia nisifufuke. Hakuna mlango angaliweza kuufunga mbele za uso wangu, kwenye asubuhi hiyo. Mihuri imevunjwa. Haleluya!

260 Mimi niko huru. Mimi ni tai. Siko katika kizimba tena, bali niko huru. Nimefufuka katika wafu, nikaingia katika

Uzima mpya wa Yesu Kristo. Si mimi peke yangu, bali kila mwanamume, wanawake, mvulana ama msichana anayeketi hapa, ambaye amejazwa katika Roho huyo wa Mungu, ni kiumbe kipya katika Kristo. Nawe ni tai.

261 Sisi tuko hai, leo, na tunafurahia ufufuo milele. Kwa kuwa Yeye yu hai, nasi tu hai, pia. Naye anaishi ndani yetu, akitufanya hai. Na Roho aliyemfufua toka katika wafu, akiishi ndani ya utu wetu, ataihuisha miili yetu ipatikanayo na mauti, katika ile Pasaka kuu ya Milele. Mungu atukuzwe!

262 Loo, chukua ulimwengu, chukua chochote unachotaka, bali unipe Yesu. Amina. Ninampenda. Yeye ni kila kitu, kwangu mimi.

263 Na kwa sababu kwamba ninyi ni sehemu Yake, mimi ni sehemu yenu, nanyi ni sehemu yangu. Na, pamoja, sisi ni sehemu Yake.

264 Loo, ewe Mkristo, ni fursa ya jinsi gani tuliyo nayo! Tuna fursa ambazo Mtakatifu Paulo hakuota kamwe angezipata. Tuna fursa ambazo Henoko, na Eliya, na wote hao hawakuwa nazo kamwe, fursa tulizo nazo sasa.

265 Na kuna maskini kondoo mmoja huko ng'ambo mahali fulani, na Yeye hataridhika mpaka huyo atakapoingia zizini. Kwa msaada wa Mungu, na kwa ono, na BWANA ASEMA HIVI, mimi ninarudi kwenda nchi za ng'ambo. Maskini kondoo huyo mdogo wa mwisho huenda akawa ni mweusi huko chini, nijuavyo mimi, ambako hao hata hawaamini kwamba wana nafsi. Bali Mungu anajua vinginevyo. Nitakwenda kutafuta mpaka siku ya mwisho wa maisha yangu, kumpata huyo, popote alipo.

266 Natumaini kamwe sijamwudhi yeyote wa ndugu zangu kwa kusema mambo haya makali. Mimi. . . Si kwamba siwatakeni mwende kanisani. Hakika, ninawataka mwende kanisani. Wewe nenda kanisani kokote unakoenda. Lakini kamwe usiache hilo liwe ndilo tumaini lako, useme, "Vema, mimi ni wa *hili*, ama mimi ni wa *lile*." Loo, ndugu, dada, kuwa wa Kristo. Nenda kanisani, bali uwe ni wa Kristo. Amina.

267 Hebu hizo—hebu hizo nguvu fiche, kama hizo hazimo ndani yako, zikuhuishe sasa hivi upate Uzima. Mbona usizipokee sasa hivi?

268 Chumba hiki kimejaa Hizo. Ninazihisi kila mahali mwilini mwangu. Ninajua Zipo hapa, zile nguvu za Mungu, yule Mwonaji mkuu wa maono, yule Mtabiri mkuu anayeweza kutabiri mambo wala kamwe hayatakosea, Yule mkuu anayeweza kunena wala hakuna mtu anayeweza kusema "sivyo," Mtu anayeweza kufungua wala hakuna mtu anayeweza kufunga. Yeye aliyekuwa amekufa sasa yu hai, na anaishi, leo, hapa Phoenix, akitembea miongoni mwa maua mapya yaliyochipuka.

269 Si ajabu, kwenye ile asubuhi ya Pasaka matone madogo ya machozi ya umande yalikuwa juu ya kila shavu la kila yungiyungi na kila waridi. Kwa nini? Lilijua lilichipushwa toka ardhini, na mahali fulani kuna ua la Milele linalonawiri. Litachukua nafasi yake siku moja. Hiyo ni kweli.

270 Si ajabu, machozi ya furaha yanaweza kutiririka mashavuni mwetu. Si ajabu, mioyo yetu inatetemeka na kutikisika tunapoweza kuhisi nguvu zizo hizo za kugeuza zikiingia maishani mwetu na kutujaza, hata kwa kutuwezesha tuzungumze katika lugha inayotoka Mbinguni.

271 Sisi tunahuishwa sana kuingizwa katika Uwepo Wake pale, kutabiri, kuona ya usoni, kubashiri, na kila kitu kikiambatana kikamilifu na Neno. Kama kitu kinatabiri kinyume na Hilo, usikiamini. Bali kama kinaambatana na Neno, limekwishasema, BWANA ASEMA HIVI.

272 "Msiogope. Mimi Ndimi niliyekuwa nimekufa, na ni hai milele hata milele." Huo ni muhuri wa Pasaka ya Mungu unaotia muhuri kila herufi ya Neno hili ndani ya moyo wako. Ule muhuri ni nini? "Ninyi ni nyaraka zilizoandikwa, zinazosomwa na watu wote." Mnajua jambo hilo. Bali wakati Mungu amekudai wewe, alikutia muhuri kwa muhuri wa Pasaka, kwamba umefufuka pamoja na Kristo, na wewe ni kiumbe kipya.

273 Kama hujatiwa muhuri asubuhi ya leo, fanya hivyo wakati tukiinamisha vichwa vyetu.

274 [Ndugu fulani anaanza kunena kwa lugha nyingine. Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]. . .Bwana. Je! mnasikia hayo? [Kusanyiko linasema, "Amina."]

275 Wazieni sasa, huku vichwa vyenu vimeinamishwa. Warumi 8:11, "Kama ikiwa kwamba Roho aliyemfufua Kristo katika wafu yuko ndani yenu, pia ataihuisha na miili yenu ipatikanayo na mauti."

276 Tunaweza kutarajia nini, enyi watu? Kuna kitu gani kilichosalia? Angalieni Formosa na ulimwengu wote. Na makombora ya atomiki na chochote kile kikiwa tu tayari kuupiga ulimwengu, na kukiweko na wasiwasi mwingi sana, na hofu, na kupiga mayowe. Na uigizaji huu wa sinema unaendelea, huko nje, wakifanya tu mizaha ya kila namna, kama tu mvulana mdogo anayepita makaburini, akipiga mbinja usiku, akijaribu kuwafanya watu waamini ya kwamba kila kitu ni shwari. Msidanganyike. Kuja kwa Bwana kumekaribia.

277 Unaona, hivi majuzi, mvuvi mmoja alikuja akaniambia, akiwa ameketi chini huko kwenye ghuba, ya kwamba, namna fulani ya kitu fulani kilichochongoka ama kitu fulani kule chini. Na jinsi ambavyo, kwamba, kipindi kirefu kabla ya lile tetemeko la ardhi kutikisa Ugiriki, samaki wote ambao kwa kawaida hula wakati huo wa asubuhi, hawakula. Ilikuwa ni kitu gani? Hawakuwa kwenye sehemu ya juu ya maji. Mara ya pili jambo

hilo lilipotukia, jambo lile lile lilitukia. Yeye alijua papo hapo jambo fulani litatukia. Hao samaki hawakuwa wakila kwenye wakati huo.

278 Na shakwe wote na kadhalika ambao huwala samaki, waliacha kula. Mapema hivyo asubuhi, huo ndio wakati wanapokula. Waliketi tu ukingoni, wakaondoka kwenye magenge na kadhalika. Kwa kuwa, katika kipindi cha dakika chache tu, kuvumwani ya baharini ilianza kuchemka kutoka ardhini, kutoka chini ya kina cha bahari. Unaona? Hao samaki walijua jambo hilo kabla halijatukia.

279 Nilipokuwa nikienda huko India, nilisoma gazeti, lililosema, “Hapana shaka tetemeko la ardhi limekwisha.” Kwa siku kadhaa, hao ndege wadogo wasingerudi kwenye viota vyao miambani. Ng’ombe wasingesimama karibu na hifadhi zao chini ya . . . kwenye kivuli, kwenye joto la mchana. Kondoo walisimama moja kwa moja huko nje malishoni, wakiegemeana. Wasingeyakaribia hayo majabali, siku mbili ama tatu kabla tetemeko la ardhi halijatokea.

280 Kwa nini? Hao kondoo walijua jambo hilo. Walijua jambo fulani lilikuwa linakaribia kutukia. Hao ndege walijua jambo fulani lilikuwa linakaribia kutukia. Hao shakwe walijua jambo fulani lilikuwa linakaribia kutukia. Hao samaki walijua jambo fulani lilikuwa linakaribia kutukia. Ni Mungu yeye yule aliyewaongoza hao wanyama wakaingia katika ile safina.

281 Hivi hamwezi kuona, ninyi watu mliojazwa na Roho, jambo fulani liko karibu kutukia? Msitarajie kitu fulani kikubwa mno cha dunia nzima, kisambae, hakuna kitu ila kule Kuja kwa Bwana Yesu. Kumbukeni, kumbukeni tu yale Maneno na ahadi ya Bwana.

282 Hivi hamwezi kuja mwingie upesi sana? Ondokeni kwenye hizo kuta kubwa. Ule ufufuo umekaribia sana sasa. Kama kuna mtu fulani hapa ambaye hajui ya kwamba wangeingia katika ufufuo huo, wala hawana uhakika ya kwamba wana nguvu hizo za ufufuo zikikaa ndani yao!

283 Ingawa mabuu ya ngozi yatauharibu, hata bomu la atomiki lilipuke moja kwa moja katikati yako, kamwe halitaziharibu hizo nguvu za kuhuisha, za kufufuka. La, la. Dada, ndugu, jina lako la thamani limeandikwa katika Kitabu cha Uzima cha Mwana-Kondoo huko juu. Hakuna mtu anayeweza kulifutilia mbali. Hakuna mchanganyiko wowote wa kutosha, ulimwenguni, kulifuta jina lako kutoka kwenye kile Kitabu Pale ambapo Damu Yake imelinunua.

284 Kama huna hakika na jambo hilo, usi—usibahatishe kwa hilo sasa. Unaona? Unaweza ukabahatisha kukimbia kupita kwenye kizuizi mahali fulani na usiuawe, bali hutapitia kwenye kizuizi hiki. La, la. Utalipata. Haitakubidi kufanya hivyo. Kuna

kimulimuli chekundu kinachomulika sasa. Vuka, vuka mawazo yako mwenyewe, vuka mambo ya ulimwengu.

285 Njoo. Hebu na tufufuliwe pamoja katika wakati huu wa fahari sana wa Pasaka, ile sherehe kuu ya Pasaka. Je! unaweza kuisherehekea moyoni mwako juma hili? Kama huwezi, je! unaweza kumwinulia Mungu mkono wako?

286 Useme, "Mungu, sina hakika na jambo hili. Sijui kama ningaliweza kufanya jambo hilo lote ama la. Je! utanisaidia? Nitakuinulia mkono wangu, Bwana. Nisaidie." Mungu akubariki. Mungu akubariki. Hilo ni jambo zuri. "Ni—ni—ninakuhitaji, Bwana. Nisaidie. Ni—ninataka—ninataka kufufuliwa. Ni—ninataka kufufuliwa. Ninataka kuwa na nguvu fiche sasa hivi. Ninataka kujua kwamba ni kweli. Ninataka kujua kwamba ni kweli, Bwana. Ninajua, siwezi kufanya ko-. . . " Hutaki kosa lolote basi. Haitakuwa . . . itakuwa imechelewa sana. Siku ndiyo hii. Jamani! Sasa siku ndiyo hii. Usingoje.

287 Si muda mrefu uliopita, nilikuwa nikihubiri. Kulikuwa na mzee mweusi aliyerudi kule nyuma ya jengo, akakutana nami. Kasema, anasema, "Kasisi, ninataka kukwambia. Ninasema unasema kweli." Akasema, "Tayari nimemwambia Bwana, muda mrefu uliopita, ninataka kushika tiketi yangu mkononi mwangu asubuhi hiyo. Ninataka kujua ya kwamba imeandikwa sahihi." Kasema, "Kutakuwako na shida nyingi kule chini mtoni." Akasema, "Ni—ni—ninashuka kwenda kule mtoni." Akasema, "Sitaki shida yoyote kule. Ninataka kuweka mambo yote sawa papa hapa." Hiyo ni kweli.

288 Je! una visa yako? Kama huna visa yako . . . Unaweza ukawa na pasipoti, lakini, kama huna visa yako, huwezi kuingia kwenye ile Nchi. Unajua jambo hilo. Je! umetayarisha kila kitu? Kama sivyo, sasa hivi ndio wakati wa kufanya jambo hilo.

289 Usiogope, kama unaogopa kidogo. Sasa, kuna kama labda mikono mia moja iliyoinuliwa hapa ndani. Kwa hiyo kama wewe unaogopa tu kidogo, sasa hebu na tulitatue jambo hilo.

290 Sasa, ninajua tuna njia mbalimbali. Wengine wanasema, "Njoo huku, hebu nikupe mkono." Wengine wanasema, "Njoo huku, piga magoti madhabahuni." Sasa, hayo ni sawa. Sina hata neno moja la kusema dhidi yake, hata kidogo, hata chembe, kitu chochote kitakachookoa.

291 Lakini hebu tu niwaambie njia yangu. "Wote walioamini, wote . . . " Kuja madhabahuni hakutakufanya uamini. Kupeana mikono na mhudumu hakutakufanya uamini. Bali kama wewe umeitwa na Mungu, nawe ni tai, kwanza, mlio mmoja tu utakwambia. Utaamini. Kama kweli unaamini hilo, nitaomba pamoja nawe.

292 Ungeweza kuwazia tai huyo mdogo kuendelea kukaa kwenye kitalu hicho zaidi? La, la. A-ha. La. Usikae hapa zaidi, ewe

rafiki. Hebu—hebu tunyakuliwe sasa. Neema ya Mungu ipo hapa kufanya jambo hilo.

293 Baba wa Mbinguni, tunatambua ya kwamba tunaelekea kwenye ile saa ya mwisho. Hatuna muda mrefu sana wa kuwa hapa sasa. Si kama umri wetu, bali kwenye ule wakati. Tunaamini kuna vijana wengi wanaoketi hapa, watakaokuwa hai wakati jambo hili litakapotukia. Huenda bado likatukia leo. Hatujui dakika wala saa. Lakini, Bwana, Wewe ulitwambia, "Mtakapoona mambo haya yakitukia," nayo yamekuwa yakitukia sasa kwa muda mrefu.

294 Tunajua tuko mbali sana, kulingana na wanasayansi. Miaka sita, saba iliyopita, tulikuwa kwenye usiku wa manane kasoro dakika tatu. Hatujui huo ni wakati kiasi gani, saa inaendelea, bali tunajua tumefika papo hapo.

295 Ee Mungu, kupata hakikisho hilo: kuona ya kwamba moyo wetu unaitikia kila ahadi ya Mungu kwa "amina," kuona kwamba Roho Mwenyewe, aliyeingia ndani yetu, anauhuisha mwili wetu.

296 Mungu, jalia ndugu zangu waone hilo, asubuhi ya leo. Jalia ndugu zangu waone hilo, ya kwamba huyo Roho anaingia na kuhuisha kwenye Neno. Jalia dada zangu waone jambo lilo hilo, Bwana. Na kisha, kama wakiona jambo ambalo halitawafanya wahuishwe kwenye Neno hilo, Ee Mungu, jalia waliondoe upesi sana. Tujalie, Baba. Yote yako mikononi mwako sasa. Ninajua ya kwamba nimekosea katika mambo mengi, na ninaendelea kukosea, lakini, Bwana, nimefanya yote nijuayo jinsi ya kufanya. Sasa liko mikononi Mwako. Hao ni Wako. Katika Jina la Yesu, wapokee, Baba.

297 Sasa kwenu ninyi mliopo hapa na mnaohitaji uponyaji kwa ajili ya mwili wenu. Ni waaminio wangapi waliopo hapa? Inua mkono wako. "Mimi ni mwaminio, kadiri ninavyoujua moyo wangu." Ni wangapi wanamiliki? Unajua, bila shaka yoyote, ya kwamba ndani ya moyo wako, sasa hivi, umefufuka katika wafu? Unajua? Loo, jamani! Ni jambo gani lingetukia katika mkutano kama huu basi? Ninajua nimechelewa, bali ni jambo gani lingetukia sasa hivi? Wazia tu kile kingaliweza kutukia. Uwezekano uko moja kwa moja ndani yako. Unaona? Wewe, uliyeinua mkono wako, umechukua kama—kama kiapo, kwa Mungu, ya kwamba, "Ninajua ya kwamba jambo fulani limenipata. Huenda nisiwe mahali pale hasa ninapopaswa kuwa."

298 Wala mimi. Hapana, bwana. Niko mbali sana na mahali ninapopaswa kuwa. Lakini ninajua jambo hili moja, nimepita toka mautini kuingia Uzimani. Ninajua jambo fulani lilinitukia. Wengi . . . Si nikiwa mzee sasa, bali miaka mingi, mingi iliyopita, lilitukia.

299 Nami ninajua, siku ile niliyoingia kwenye ile hospitali, wakati nilipopata changamoto yangu kubwa. Nilimwona mke wangu akifa; mimi nikiyaombea maisha yake. “Basi nimefanya nini ila kusimama kwenye pembe ya barabara, kuhubiri, na kuwaombea wagonjwa?”

Na ndipo Shetani akasema, “Vema, Yeye hatayajibu maombi yako.”

300 Nilimwona akifa, bali ninajua ya kwamba ndani yake kulikuwako na zile nguvu za ufufuo. Mifupa hiyo itafufuka tena.

301 Nilimwona mtoto wangu mchanga amelala pale. Nami nikaweka mkono wangu juu yake, nikasema, “Mungu, usimchukue.”

302 Inaonekana kana kwamba alishusha pazia chini, akasema, “Hata sitakusikia tena.”

303 Shetani akasema, “Haya basi. Neno moja tu . . . ” Alijua vizuri zaidi asingeniambia hakuna Mungu, maana nilijua hilo. Lakini alisema Yeye hanipendi, hanijali. Unaona? Kila jambo la hoja, kasema, “Wewe ni kijana mwanamume tu, bado hujafikia umri wa miaka ishirini. Huyo hapo mke wako amelala hapa katika nyumba ya maiti. Na huyu hapa mtoto wako mchanga akienda huko. Na—na ninii tu . . . Ulisema Yeye alikuwa Mponyaji mkuu, na Yeye ni *haya* yote. Basi, angalia, Yeye anafanya nini? Neno moja, hata haingemlazimu kulinena, ni kuangalia tu chini pale na kutamka. Kutikisa tu kichwa Chake, hilo tu ndilo lingetukia, naye angepona. Lakini, unaona, Yeye hakupendi. Hakujali. Anamwacha mtoto wako afe hapo sasa hivi, na hata anakataa kusikia maombi yako katika saa hii ya huzuni.”

304 Kila kitu alichosema kilikuwa ni kweli kabisa. “Kwa hiyo wewe umefanya nini? Siku nzima unashughulika, mpaka ingekuwa ni vigumu kwako kusimama. Na halafu unakaa macho usiku kucha, mpaka saa sita na saa saba. Unasimama kwenye pembe za barabara, ukihubiri. Ukitembelea hospitali. Unakuja tu na kuketi, kitini, unaketi pale na kulala saa moja ama mbili, kisha unarudi kazini tena. Kesho yake usiku, jambo lile lile. Nawe huyu hapa, ukiwa na umri wa kama miaka ishirini na moja, ishirini na mbili. Kila rafiki, kila msichana, kila mvulana uliyewahi kushirikiana naye, alikuita mwendawazimu asiye na akili. Kwani umefanya nini? Umejipumbaza. Hivi huoni hilo?” Nilikuwa niko karibu tu kukubaliana naye.

305 Ndipo kitu Fulani ndani yangu, hicho kilikuwa ni ile nguvu ya kuhuisha. Nikasema, “Bwana alitoa, na Bwana ametwaa. Jina la Bwana libarikiwe.”

> Matumaini yangu yote yanapokwisha,
> Basi Yeye ndiye tumaini langu lote na nanga
> yangu.

Kwa kuwa katika Kristo, ule . . .
[Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] . . . mchanga unaodidimia.

Loo, atakuja na sauti ya ushindi,
Jalia basi nipatikane nda—ndani Yake,
Nimefunikwa na mavazi ya haki Yake.

306 Si katika haki yangu; sina yoyote. Yangu ni matambara machafu, yenye kinyaa. Ningechukia kujaribu kuingia Mbinguni kwa kuhubiri kwangu. Ningechukia kujaribu kwenda Mbinguni kwa maono yangu. Ninaenda Mbinguni kwa kuwa ninashikilia neema Yake moyoni mwangu. Neema Yake, hiyo ndiyo sababu ninakwenda. Hivyo ndivyo tunavyoenda.

307 Loo, ewe rafiki, wewe ni sehemu ya Mwili huu. Ninyi ni watoto wadogo wa Mungu. Sasa, ninasema jambo hili kujenga tumaini lenu. Kama ulipata . . .

308 Kama nimepata kibali kwenu, nimewaambia Kweli. Na yale nimewaambia, ni—ni vile alivyosema nabii, miaka kadhaa iliyopita. Si kujifanya nabii Wake. La, bwana. Lakini ninawaambia Kweli. Je! hivi Yeye amewahi kusema jambo lolote ila lililokuwa ni kweli? Nimewajua ninyi sasa kwa muda wa miaka ishirini na kitu, hapa Phoenix, tangu ule wimbo, *Ningependa Kulizungumza Nay*e *Kwa Undani*, kule kwenye kanisa la Ndugu Outlaw, ninaamini ilikuwa ni huko, na Ndugu Garcia. Je! nimewahi kuwaambia jambo lolote katika Jina la Bwana ila lile lililotukia?

309 Kumbukeni, kuna tumaini moja tu. Pateni nguvu hizi za kuhuisha. Zitawashikilia. Wakati kila kitu kimeachilia, hizo zitakushikilia.

310 Baadhi yao walisema, "Je! ulishikilia dini yako, Ndugu Branham?"

Nilisema, "Hapana. Ilinishikilia."

311 Hunishikilia. Si mimi ninaishikilia. Si suala la mimi kushikilia, ama kutoshikilia. Ni kama Yeye alishikilia, ama hakushikilia. Yeye ndiye aliyeshikilia kwa ajili yangu.

312 Haikumlazimu kufanya hivyo. Malaika walikuwa wameketi kwenye kila mti, wakasema, "Hebu nyosha tu vidole vyako. Elekeza tu; si lazima kuuchukua toka msalabani. Hebu elekeza tu kidole chako, uone ni kitu gani." Unaona, kundi hilo lenye kudhihaki. Lakini kama angelifanya hivyo, nisingekuwa na ushuhuda huu leo hii; usingekuwa nao. Lakini kwa sababu Yeye alikaa msalabani, alishikilia pale, hiyo ndiyo sababu mimi ninashikilia pamoja Naye.

Kwake Yesu, Mwamba wenye imara, nasimama;
Ardhi zingine zote ni mchanga udidimiao.

313 Sasa, kama wewe ni mgonjwa, naomba mwekeane mikono. Na tuombe. Weka tu mikono yako juu ya mtu aliye karibu nawe. Haidhuru una shida gani, amini sasa. Kama nilipata kuwaambieni Kweli, ninawaambia sasa. Mnaona? Yesu alisema, "Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio." Nanyi ni waaminio, inueni tu mikono yenu. Msitie shaka. Kuna maskini mtu anayeumwa ambaye umemwekea mikono. Mtu fulani ameweka mikono yao juu yako.

314 Kumbukeni nguvu hizo za kuhuisha, nguvu hizo zilizomfufua Yesu kutoka kaburini. Sasa uwe na imani katika kile ulicho nacho mwilini mwako—mwako mwenyewe. Itamsaidia mtu huyo ambaye umemwekea mikono yako. "Kama anakaa ndani yenu, ataihuisha pia miili yenu ipatikanayo na mauti."

315 Mungu mpenzi, ninaposimama hapa asubuhi ya leo, ikikaribia wakati wa adhuhuri, wakati ni karibu na saa hii siku ambayo Yesu alilia, "Mungu Wangu, Mungu Wangu, mbona umeniacha? Ninaona kiu." Si ajabu, nabii alitangulia kuona jambo hilo, na akasema, "Mifupa yangu yote, imeteguka. Walinizua mikono na miguu Yangu." "Bali alihesabiwa pamoja na wakosaji. Bali alijeruhiwa kwa makosa yetu. Alichubuliwa kwa maovu yetu. Adhabu ya amani yetu ilikuwa juu Yake, na kwa kupigwa Kwake tumepona." Tunadai jambo hilo, asubuhi ya leo, Mungu. Tunadai hilo.

316 Katika asubuhi ya ufufuo huu, angalieni, Ukweli huu uliothibitishwa niliosimulia, Bwana, kutoka kwenye Neno Lako, Mbele za Mungu. Yeye ni Hakimu, nasi tu mashahidi kwamba Yeye ametukomboa. Na ndani yetu mnakaa, kwa neema ya Mungu, zile nguvu za kufufuka. Na marafiki zetu ni wagonjwa, yule ambaye amewekewa mikono.

317 Ee Mungu, tunamsai Ibilisi, katikati ya imani yetu asubuhi ya leo, watu wakiwa wamewekewa mikono, na mikono yangu ikiwa imenyoshwa juu ya watu. Jalia kila ugonjwa, kila mateso yanayojaribu kuwashikilia watu, katika uwepo wa Kweli hii iliyothibitishwa, yaondoke. Katika Jina la Yesu Kristo, jalia watu hawa wawekwe huru leo. Kwamba, Biblia, Maneno ya Mungu wetu yalisema, "Wakiweka mikono yao juu ya wagonjwa, watapata afya." Na mikono yetu ilikwishainuliwa juu hewani, kuelekea Kwako, Mungu.

318 Kama, kila mmea wa duniani unavyokunywa kwenye chemchemi Yako. Na kwa hakika kama vile mmea huo, ambao umepewa uhai, unavyokunywa toka kwenye chemchemi Yako, unaanza kujijenga. Unaanza kukua. Shina la mhindi, ua, chochote kile kinachokunywa kwenye chemchemi Yako, kinakua kikielekea Kwako.

319 Na asubuhi ya leo, tumekua, inchi kadhaa, Bwana. Tunaweza kufika juu zaidi. Tunakunywa kisimani Pako. Sisi ni

viumbe Vyako, tukiwa na nguvu za kufufuka ndani yetu, Bwana. Nasi tunaomba ya kwamba utayasikia maombi yetu kwa ajili ya ndugu na dada zetu. Na jalia kila mateso, ambayo yanawazuia watu hawa wapendwa hapa ambao wana nguvu hizi, Bwana, wafunguliwe, wapate kumtumikia Mungu. Na itakuwa ni vema, Bwana. Katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

320 Mnamwamini? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Ati uache kitu kama hiki? Unawezaje kufanya hivyo? Inakubidi tu, inavyoonekana, kujiondoa tu. Je! unajisikia hivyo? ["Amina."] Mimi—mimi—mimi. . .Huenda ikawa tu kwamba ni mimi, ambaye ninaninii. . .Bali nilikuwa nikihisi, hisia ngeni tu nilipokuja miongoni mwa watu, ambapo mliketi pamoja namna hii. Ninajua, mahali fulani, pasipoonekana hapa; kama tu vile redio, televisheni, chochote kile, kinachopitia humu chumbani; Kristo yuko humu chumbani. Wazia tu, Mkombozi wetu! Tony, Yeye yupo hapa. Amina.

321 Na ni nani angeliweza kuwa na furaha zaidi kuliko watu wanaomiliki, kwa ushuhuda wa Biblia wa kila Neno la Mungu likidhihirishwa, kuona hata Malaika pamoja na Utu Wake, kama walivyofanya kote katika nya—nyakati! Na hapa, Maneno ya waonaji, yaliyotabiri na yakatukia vivyo hivyo kabisa. Nasi tupo hapa kwenye mkesha wa Kuja Kwake. Loo, ni wakati wa fahari jinsi gani!

322 Tutamwona. Moja ya siku hizi, Yeye atakuwa hapa. Mpaka atakapokuja, je! mtaniombea? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Nina maafa ya hatari kubwa mbele zangu. Ninajua hilo. Unaona? Nami ninakutana na makafiri ambao wangeweza kukupiga risasi, mamoja kama tu kunywa maji, nawe unalipiwa tu. Ukienda kwao, pepo watakaokupa changamoto juu ya Biblia, kwa urahisi tu hivyo. Lakini kamwe sijaona wakati ila ambapo Mungu wetu alipata ushindi. Ninaenda katika Jina Lake, katika Jina la Bwana Yesu Kristo, tumaini la Uzima wa Milele, ufufuo na Uzima. "Yeye aishiye na kuniamini Mimi, ajapokufa hata hivyo ataishi. Naye aishiye na kuniamini Mimi hatakufa kamwe." Ninaamini hilo kwamba ni Neno la Mungu la Milele. Je! ninyi mnaamini vivyo hivyo? ["Amina."] Mtaniombea? ["Amina."] Nitawaombea. Mungu na atulinde hata tutakapokutana tena.

323 Sasa hebu na tusimame kwa miguu yetu, kwa dakika moja. (Una jambo lolote unalotaka kusema?)

Na tuinamishe vichwa vyetu.

324 Isingekuwa sawa kwetu kutoimba wimbo huu mfupi, sivyo? Je! mnaukumbuka wimbo wetu, *Nampenda*, je! huo uko kwenye kila moyo? Hebu na tuuimbe tu. Dada, mpendwa, ungeweza. . . Ninataka kusema, ninapendezewa na kupiga kwako, pia, dada. Vema.

Nampenda, nampenda
Kwani alinipenda kwanza
Na kununua wokovu wangu
Mtini Kalvari.

Sasa tutaenda kuubadilisha wimbo.

Imani yangu inakuangalia Wewe,
Ewe Mwana-kondoo wa Kalvari,
Mungu Mwokozi;
Sasa nisikie niombapo,
Loo, ondolea mbali maovu yangu yote,
Loo, nijalie tangu leo
Kuwa wako kabisa!

325 Je! huo hauwafanyii jambo fulani? Ni wangapi wanaopenda huo moyo halisi...Mimi—mimi—mimi ninapenda nyimbo za yubile. Hakika, ninazipenda. Lakini wakati ukiwa katika roho wa kuabudu, hivi hampendi hizo nyimbo za kale za dini? Ninaamini Roho Mtakatifu alimvuvia Eddie Perronett na hao ambao waliandika nyimbo hizo nzuri za kale. Hivi hamwamini hivyo? Fanny Crosby, wakati alipoandika.

Usinipite, ewe, Ee Mwokozi mpole
Sikia kilio changu kinyenyekevu;
Unapozuru wengine,
Usinipite.

Wewe ndiwe chemchemi ya faraja yangu yote,
Zaidi ya uhai kwangu,
Ni nani niliye naye duniani mbali na Wewe?
Au ni nani mbinguni ila Wewe?

326 Huo si ni mzuri sana? Hilo linatufanya tutake kuimba *Nampenda*. Sivyo? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Sasa, tunapoimba wakati huu, *Nampenda*, hebu...Tunapendana. Ikiwa hatupendani, basi hatuwezi kumpenda Yeye. Sasa hebu na tupeane mikono. Hebu simameni tu, na unyoshe mkono juu ya meza mahali fulani, mkapeane mikono, mmoja kwa mwingine.

Na...[Ndugu Branham anaondoka kwenye kipaza sauti na kuzungumza na mtu fulani—Mh.]
Na kununua wokovu wangu
Mtini Kalvari.

Na tuinamishe kichwa chetu sasa.

327 Nitamwomba Ndugu Williams, Ndugu Williams mdogo, aje hapa kwa dakika moja. Nitamwomba kama anaweza kuwaruhusu wasikilizaji hawa wafumukane katika maombi.

328 Ninampenda Ndugu Williams, Mkristo mchanga, ambaye ninafikiri kweli ni mtumishi wa Kristo, familia yake ndogo. Nina ushirika mwingi sana pamoja na hawa. Na hao vijana wa thamani wa Moseley na hao wote, tumekuwa pamoja,

na wengi sana wa marafiki zangu wapendwa hapa Phoenix, ninaowapenda kwa moyo wangu wote. Ninafikiri, asubuhi ile katika lile ono, Yeye alisema, “Wote uliowahi kuwapenda, na wote wanaokupenda, Mungu amekupa.”

329 Ninaamini mtu fulani hapa anatubu dhambi yao, hapa sakafuni, msichana akilia.

Hebu na tuinamishe vichwa vyetu kwa dakika moja kwa ajili yake.

330 Mungu mpenzi, je! huyo ndiye yule kondoo mdogo aliyesalia katika Phoenix? Sijui, Mungu. Wewe unajua. Lakini, siku moja, itakuwa ni hivyo. Lakini, Baba, huyu, bila shaka, ni mmoja. Kwa hiyo ninaomba ya kwamba Wewe ungemsaidia, sasa hivi tu. Kwa upendo fungua lango, useme, “Njoo, Mwanangu. Ingia kutoka kwenye barabara ya uchovu, yenye usumbufu. Umekuwa ukijikwaakwaa huko gizani. Nimetoka, leo, kuja kukuchukua. Roho Wangu Ndiye anayenena nawe na kukuingiza kwenye zizi sasa.” Tujalie, Mungu. Jalia msichana huyu . . . akiwa tu kwenye njia panda ya maisha hapa. “Yeye atakayeyasikia Maneno Yangu, na kumwamini Yeye aliyenipeleka, yuna Uzima wa Milele.” Mjalie, Mungu mpenzi, Mkristo huyu mchanga. “Yeye atakayekuja Kwangu, sitamtupa nje kamwe.” Wakati watakatifu wanasimama pande zote za msichana huyu, wakiomba.

331 Kumbukeni, hata Paulo, aliyepigwa mawe vibaya sana hata alikuwa yuafa, na wakati ninii . . . ? . . . watakatifu waliposimama pale na kuomba, uhai ulimrudia. Kwa sababu, katika miili hiyo ya hao watakatifu kulikuwa na nguvu hizo za kuhuisha zilizoirudisha roho ya uhai kwa Paulo. Mungu, hakika ingeweza kuomba ombi, la mauti kutoka . . . ama mauti kutoka kwa mtu huyo, kwa maombi ya imani, kupata uzima. Tujalie, Mungu mpenzi.

332 Tubariki sasa tunapokungojea Wewe. Katika Jina la Yesu Kristo, tunaomba.

333 Sasa huku vichwa vyenu vimeinamishwa, nitamwomba Ndugu Williams.

*Muhuri Wa Pasaka* SWA65-0410
(The Easter Seal)

Ujumbe huu uliohubiriwa na Ndugu William Marrion Branham, uliotolewa hapo awali katika Kiingereza mnamo Jumamosi asubuhi, tarehe 10 Aprili, 1965, kwa ajili ya kiamshakinywa cha Ushirika wa Kimataifa wa Wafanyabiashara wa Full Gospel katika Hoteli ya Ramada huko Phoenix, Arizona, Marekani, umetolewa kwenye kanda ya sumaku iliyorekodiwa na kuchapishwa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice Of God Recordings.

SWAHILI

©2015 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

## Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org